

**KILIMO**
Halmashauri ya Majani Chai yahimizwa kutumia njia mbadala kutatua mzizo Uk 2



**MADINI**
Serikali kuchunguza leseni kwenye msako dhidi ya wawekezaji matapeli UK 3

**MIPANGO**
Mfumo wa uzoaji maji taka mjini Narok uliogharimu 1.7 bilioni tayari kwa uzinduzi



Uk 8

www.mygov.go.ke

JANUARI 10, 2023

TATHMINI YAKO YA WIKI

# MyGov.

TOLEO No. 26/2022-2023

**Takwimu za Wiki**

**43**
Miaka ambayo bomba la mafuta ambalo KPC itakoma kulitumia limekuwa likisafirisha mafuta

**312**
Wasichana ambao wamejiunga n makao ya watoto na nyumba salama eneo la Kuria

**.1963**
Mwaka ambapo kituo cha mafuta cha Kipevu Oil Terminal kilijengwa katika bandari ya Mombasa

**64,000**
Ekari za ardhi zinazomilikiwa na Kishushe Ranching Cooperative Society Ltd

**12,000**
Ekari za ardhi ambapo mradi wa unyunyiziaji maji mashamba wa Tana Delta unaendeshwa.

AFYA

# Madaktari wakufunzi 800 kutumwa hospitalini

Waziri wa Afya Dkt Susan Wafula asema kwamba hatua ya hivi punde ya serikali inalenga kutatua tatizo la uhaba wa madaktari wa matibabu katika hospitali za umma nchini

**NA KIPTANUI CHERONO (KNA)**

Zaidi wa madaktari wakufunzi 800 watatumwa katika hospitali za umma kote nchini katika wiki mbili zijazo kuinua utoaji wa huduma za afya.

Waziri Afya Dkt Susan Wafula anasema kwamba hatua ya hivi punde ya serikali inalenga kutatua tatizo la uhaba wa madaktari wa matibabu katika hospitali za umma nchini.

Akizungumza akiwa Hospitali ya Mafunzo na Rufaa ya Moi, Eldoret, Waziri Wafula alisema kwamba serikali imejitolea kuhakikisha kwamba vituo vyote vya afya viko na wafanyakazi na ujuzi 3wa kutoa afya kwa wote kwa raia.



**Waziri wa Afya Susan Wafula akihutubu wakati wa ziara yake katika Moi Teaching and Referral Hospital, Eldoret**

ENDELEA UK 2

# KPC yaacha kutumia bomba lililojengwa miaka 43 iliyopita

**NA MUTISO MBITHI (MYGOV)**


Kampuni ya Bomba la Mafuta ya Kenya (KPC) itaondoa bomba la inchi 14 ambalo liliacha kutumika tangu Desemba 2021 baada ya kupitisha bidhaa za mafuta kutoka jiji la pwani la Mombasa kwa miaka 43.

Line One ( kama lilivyofahamika bomba lililojengwa 1978) ambalo limekuwa likibeba mafuta kutoka Mombasa hadi Nairobi, halitatumika kutoa nafasi kwa mpya la Line Five la inchi 20 kuanza kusafirisha bidhaa za mafuta kutoka Mombasa hadi Nairobi, Eldoret na Kisumu kwa zaidi ya wauzaji 100 wa mafuta wanaohudumiwa na KPC.

Baada ya kuacha kutumia Line 1, maafisa wa KPL walifichua kwamba kampuni itachimbua bomba hilo la nchi 14 na kuuza kama chuma kikuukuu

Maafisa hao waliongeza kuwa, hata hivyo, kilomita 279 vya bomba la zamani zitauzwa kama chuma kikuukuu huku kilomita 171 zitakazobaki kutoka Mombasa hadi Mtito Andei zitachukuliwa na kampuni ya maji ya Mombasa kuteka na kutoa maji kutoka chemi chemi ya Mzima Springs hadi Pwani ya Kenya.

"Tutabadilisha Line 1 kutoka bomba la mafuta kuwa la kubeba maji kutoka Mzima Springs hadi Mombasa ili kusaidia bomba la maji linalobeba maji hadi Mombasa ambalo lilijengwa 1953 na hivyo basi kuimarisha usambazaji wa maji katika pwani," afisa wa KPC aliambia wanahabari katika kituo cha Mtito Andei.



**Matanki ya Kenya Petroleum Refineries, Mombasa**

Line 5, ambayo ni mpya iliyogharimu Sh48 bilioni na ambayo ilianzishwa 2018, ina uwezo wa kusafirisha lita 1 milioni za mafuta kwa saa.

Afisa huyo wa KPC aliongeza kuwa kampuni inanuia kuboresha Line 5 mchakato wa kuondoa Line 1 utakapokamilika kuiwezesha kusafirisha lita 1.8 milioni za mafuta kwa saa kutoka Mombasa.

Maafisa wa KPC wanaosimamia vituo tofauti kwenye Line 1 walisema kwamba mpya la Line 5 itasaidiwa na pampu mpya ambayo itakuwa sambamba nayo kuongeza mtiririko ili iweze kusafirisha mafuta kwa kasi.

"Uwezo wake utakapoimarishwa, KPC itatwaa soko la mafuta la Afrika Mashariki na Kati kwa kusafirisha bidhaa zaidi hadi Eldoret na Kisumu," meneja wa KPC alisema.

Afisa huyo aliongeza kuwa KPC pia ina mpango wa muda mrefu wa kuwa na maeneo zaidi ya kuhifadhi mafuta katika kaunti zote 47 Kenya kando na kupanua bomba hadi kaunti zote.

KOMESHA COVID-19

“Virusi havitembei, watu huvisambaza, tukiacha kutembea, virusi vitakufa”




# Madaktari wakufunzi 800 kutumwa hospitali za umma

ENDELEA UK 1

Wafula ambaye alikuwa katika ziara yake ya kwanza kujifahamisha na vituo vya afya za umm aliambia Chama cha Madaktari na Wataalamu wa Meno kusubiri huku serikali ikishughulikia malalamishi yao badala ya kutoa vitisho .

Kauli zake zilijiiri maafisa wa chama cha madaktari wakitishia kuitisha mgomo kuhusu kukosa kwa serikali kuajiri madaktari wakufunzi.

Maafisa hao wakiongozwa na Katibu Mkuu Dkt Davji Atellah walikuwa wametoa ilani ya mgomo ya mwezi mmoja kuhusiana na malalamishi kadhaa yanayojumuisha kuajiriwa kwa madaktari hao wakufunzi katika hospitali za umma nchini.

“Serikali haitaki vitisho kutoka kwa vyama vya madaktari, tunachojali ni utoaji wa huduma za afya kwa wote na kuajiri madaktari wakufunzi zaidi katika hospitali zetu,” alisema Wafula, ambaye alikuwac ameandamana na Afisa Mkuu Mtendaji wa hospitali hiyo Dkt Wilson Aruasa na Gavana wa Uasin Gishu Jonathan Bii.

Waziri alipuuza madai kwamba Mpango wa Linda Mama umefutwa na utawala wa sasa.

Aliongeza kuwa mpango huo, aliosema ni mzuri, hautaondolewa.

“Ninajua kumekuwa na maneno katika vyombo vya habari kwamba Linda Mama imefutwa, lakini ninataka kuwathibitishia kwamba kama Waziri wa Afya Linda Mama iko, akina mama wote wajawazito wanashughulikiwa na

Linda Mama,” alisema.

Waziri alipongeza MTRH kwa kuwa taasisi ya kuigwa katika utoaji wa huduma za afya kwa Wakenya.

Waziri alisema kwamba serikali imejitolea kujenga jengo la vitanda 2000 katika MTRH eneo la Kiplombe, karibu na uwanja mdogo wa ndege wa Eldoret.

Wafula aliahidi kufanya mageuzi katika Hazina ya Bima ya Afya ya Taifa (NHIF) na katika Shirika la Usambazaji wa Dawa na Vifaa vya Matibabu Kenya (KEMSA), huku akishirikiana kwa karibu kikazi na serikali za kaunti katika utoaji wa huduma za afya, hasa afya ya msingi (PHC).

Akizungumza katika hafla hiyo, Gavana wa Uasin Gishu Jonathan Bii alisifu uhusiano mwema wa kikazi na MTRH katika masuala ya afya, na akaeleza shukrani zake kwa AMPATH Revolving Pharmacy ambayo imerudi kuhudumu katika vituo vya afya vya kaunti hiyo.

# Bodi ya Chai ya Kenya yahimizwa kutumia njia mbadala kutatua zogo

NA CATHERINE MUINDI (KNA)

WAZIRI wa Kilimo na Ufugaji , Bw Mithika Linturi, ameagiza Bodi ya Chai ya Kenya (TBK), kushirikiana na wakurugenzi na wadau wengine kutumia njia mbadala za kutatua mizozo ili kusuluhisha kesi zilizopo na kufanikisha utekelezaji wa Sheria ya Chai ya 2010.

Akizunguza katika mkutano wa kila mwaka wa wakurugenzi wa KTDA, Bw Linturi alisema kesi nyingi zilizo kortini kupinga sheria hiyo, zimelemaza utekelezaji wa baadhi ya mageuzi.

Linturi alihimiza shirika hilo kushirikiana na wakurugenzi na wadau wengine kutatua masuala yanayozozaniwa, akisema kwamba kuna kesi nyingi zinazopinga utekelezaji wa Sheria ya Chai ambazo zimelemaza utekelezaji wa baadhi ya mageuzi na uafikiaji wa matokeo yaliyonuiwa. Akizungumza katika kongamano la kila mwaka la wakurugenzi wa KTDA Linturi alisema kwamba wakati sheria hiyo itatekelezwa kikamilifu, baadhi ya vipengeee vya sehemu ya 54 ya Sheria ya Chai ya Kenya 2020, inayoanzisha Hazina ya Chai, vitaanza kutumika.


Waziri wa Kilimo na Mifugo Mithika Linturi akipokea zawadi kutoka kwa mwenyekiti wa KTDA Holdings David Muni Ichoho wakati wa mkutano wa kila mwaka wa wakurugenzi wa Kenya Tea Development Authority (KTDA) katika Kenyatta International Convention Center (KICC), Nairobi.

Hazina ya Chai, alieleza, itatumiwa kuthibiti bei ili kukinga wakulima dhidi ya kushuka kwa bei. Pesa hizi zitatoka kwa ushuru wa Chai miongoni mwa vyanzo vingine vilivyotajwa chini ya sheria hiyo.

Hata hivyo, Linturi alisema kwamba ukusanyaji wa ada hizo unalemazwa na kesi kortini zinazosimamisha utekelezaji wa sehemu ya 53 ya sheria ya chai na akahimiza walalamishi kubadilisha msimamo wao na kuondoa kesi hiyo miongoni mwa zingine dhidi ya Sheria ya Chai, 2020 kwa lengo la kuendeleza sekta hiyo mbele. Waziri alisema kwamba miongoni mwa hatua za kushughulikia gharama ya juu ya pembejeo na kukinga wakulima wa chai kutokana na kupanda kwa bei ya mbolea ni kuweka ruzuku ya mbolea.

“Katika mwaka huu wa kifedha, serikali ilitoa ruzuku ya mbolea ya Sh4.44 bilioni kwa wakulima wa chai katika viwanda vyote 24 vya wakulima wa mashamba madogo. Hii ilipunguza bei ya mbolea kwa Sh 2,117 kwa gunia ya kilo 50. Inatarajiwa kwamba kufuatia kutumiwa kwa mbolea wakati wa mvua ya vuli, uzalishaji na ubora wa chai utaimarika na kuimarisha mapato ya wakulima,” alisema waziri.

## HIGHER EDUCATION LOANS BOARD
## ADVERTISEMENT OF VACANT POSITIONS

**Join our team and contribute to our effort of making education more accessible to Kenyans**

The Higher Education Loans Board (HELB) was established in 1995 through an Act of Parliament CAP 213A of the laws of Kenya. The mandate of HELB is to source for funds and provide financing (through loans, scholarships and bursaries) to Kenyans pursuing higher education in institutions of higher learning in and outside Kenya as recognized by Commission for University Education (CUE) and/or the Technical, Vocational Education and Training Authority (TVETA), and recover funds loaned to create a National Revolving Fund. HELB is an innovative institution in the education sector whose focus is to leapfrog how Financing higher education is executed in Kenya by amalgamating public and private sector resources in the country.

HELB is seeking to recruit competent, self-driven individuals with an innate dynamism for the three (3) positions listed below. The successful candidates to fill the positions will join a highly performing team and should not only be passionate, innovative, and qualified, but also be of integrity, dependable, emotional intelligence, effective interpersonal, communication and leadership skills.

### 1 Assistant Manager Research, Strategy and Planning – Grade 4

The job holder will be responsible for:

- Coordinating the implementation of policies and procedures for efficient and effective strategic plan formulation.
- Research, Quality Management, Performance Contracting.
- Performance Management, Monitoring and Evaluation.
- Knowledge Management and Business Process Re-engineering.
- Formulation and review of the Strategic Plan for the Board.

### 2 Assistant Manager, Internal Audit – Grade 4

The job holder will be responsible for:

- Coordinating conduct of various types of audits and reviews in accordance with International Standards for professional practice of Internal Auditing.
- Promote efficiency and effectiveness of operations, reliability and integrity of financial and operational information.
- Safeguarding assets and to ensure adherence to applicable laws and regulations, policies and procedures, standards and contracts for the Board.

### 3 Senior Legal Officer, Litigation and Prosecutions – Grade 5

The job holder will be responsible for:

- Formulating, reviewing and monitoring statutory and legal policies and procedures relating to litigation, prosecution and alternative dispute resolution processes for the Board.

**For detailed Job Descriptions and application procedure, please visit HELB website : www.helb.co.ke.**

The deadline for receiving applications is **Tuesday, 31st January 2023 through** Email Address: **recruitmenteja@helb.co.ke**

Successful candidates shall be required to prove their compliance with Chapter 6 of the Constitution of Kenya, 2010 by obtaining and presenting clearance/compliance certificates from the following Institutions:-

1. Kenya Revenue Authority;
2. Higher Education Loans Board;
3. Ethics and Anti-Corruption Commission.
4. Directorate of Criminal Investigations (Certificate of Good Conduct) and
5. Credit Reference Bureau.

**HELB is an equal opportunity employer. Persons with disabilities are encouraged to apply.**
**Only shortlisted candidates will be contacted.**

**EMPOWERING DREAMS**

www.helb.co.ke Anniversary Towers University Way **USSD** *642# +254711052000 contactcentre@helb.co.ke @HELBPAGE

## HIGHER EDUCATION LOANS BOARD
## TENDER ADVERTISEMENT
## OPEN NATIONAL TENDER

The Higher Education Loans Board is a state corporation whose mandate is to source for funds and provide loans, scholarships and bursaries to Kenyans studying in recognized institutions of higher learning.

HELB invites interested, reputable firms with experience for the submission of sealed tenders as follows:-

| Tender Number | Tender Description | Tender closing date | Eligibility |
|---|---|---|---|
| HELB/T/09/2022-2023 | Supply, Delivery, Installations and Commissioning Blade Servers, SAN System and Backup Replication Solution | Tuesday 24th January 2023 at 11.00 a.m. | Open |

Interested and eligible firms may obtain further information and inspect the tender documents at the Procurement office on 18th floor of Anniversary Towers, University Way, Nairobi, during normal working hours or view and download the respective **detailed tender advert** and **tender document** from our website **www.helb.co.ke/procurement/** or **https://tenders.go.ke.**

All bidders interested in participating in the tender must notify HELB of their participation in the tender by emailing their contact details to **procurement@helb.co.ke** in case of any further tender addendum.

**EMPOWERING DREAMS**

www.helb.co.ke Anniversary Towers University Way **USSD** *642# +254711052000 contactcentre@helb.co.ke @HELBPAGE

Funika mdomo unapopiga chafya
20 SEC Nawa mikono na sabuni/ Sanitaiza
Jitenge na walio na virusi
Usiguse macho, pua au mdomo na mikono michafu
Pika nyama na mayai ziive. Usile chakula kibichi
Hakikisha maeneo yote ni safi
KOMESHA COVID-19
UZUIAJI


# Serikali kuchunguza leseni za uchimbaji madini kuondoa wawekezaji matapeli

**NA WAGEMA MWANGI (KNA)**

Serikali itaanza kuchunguza uhalali wa leseni zilizotolewa kwa kampuni za uchimbaji madini kote nchini kutekeleza uzingatiaji na kuleta mpangilio katika sekta hiyo ya mabilioni ya pesa. Waziri wa Madini, Uchumi wa Baharini Salim Mvurya alisema kwamba hakuna kampuni itakayoruhusiwa kuhudumu Kenya ikiwa na leseni iliyopita wakati wake au bila kutoa stakabadhi halali zinazotambuliwa na sheria. Waziri alikuwa akizungumza katika Kishushe baada ya kutembelea kampuni inayoyokumbwa na mzozo ya Samruddha Resources Kenya Ltd, inayoongoza kwa uchimbaji wa madini ya chuma katika kaunti ya Taita Taveta.

> Nimebuni kundi la kuharakisha mchakato wa kulainisha namna ya kugawa mapato," -Mvurya



**Waziri wa Madini na Uchumi wa Baharini Salim Mvurya (kulia) alipotembelea kampuni ya Samruddha Resources Kenya Ltd**

Alikuwa akiandamana na maafisa wakuu akiwemo Katibu wa Masuala ya Baharini Shedrack Mwadime na mwenzake wa Madini Irungu Mwangi. Viongozi waliokuwemo walijumuisha Gavana Andrew Mwadime, Kamishna wa Kaunti Loyford Kibaara, wabunge Danson Mwashako (Wundanyi), Peter Shake (Mwatate) John Bwire (Taveta), Senator John Mwaruma Mwakilishi wa Kike Lydia Haika

"Tutakagua leseni zilizotolewa kwa wachimbaji madini ili kuhakikisha ziko sawa. Enzi ambazo wachimbaji madini walikuwa wakiendesha shughuli zao katika kaunti bila kuwa na leseni halali zimeisha," alisema. Mvurya alisema kwamba kampuni za uchimbaji madini lazima zizingatie sheria ya Madini ya 2016 hasa katika ugavi wa mapato.

Sheria aliyotaja inasema kuwa asilimia 70 ya mapato kutoka kwa uuzaji wa madini inafaa kuwa ya Serikali ya Kitaifa, huku asilimia 20 ikifaidi serikali ya kaunti ambayo kampuni ya madini inahudumu. Jamii inayoishi eneo la uchimbaji madini inapaswa kupata asilimia 10.

Waziri alisema kwamba ugavi wa mapato kutoka kwa uuzaji wa madini miongoni mwa makundi hayo matatu umeathiriwa na ukosefu wa sera za wazi na mfumo kazi wa sheria wa kuwezesha utoaji wa pesa.

Alifichua alikuwa ameunda kundi la kuharakisha shughuli za ugavi wa mapato ili kuwezesha Wizara ya Fedha kutoa pesa kwa serikali ya Kaunti. "Nimeunda kundi la kuharakisha mchakato wa kunyoosha ugavi wa mapato. Kundi hili litafanya kazi kwa karibu na maafisa kutoka serikali za kaunti ili kuhakikisha mirahaba ya madini inatolewa kwa kaunti," alisema.

# Shirika laimarisha juhudi za kurudisha wanaotoroka FGM Migori katika jamii

**NA GEORGE AGIMBA NA GEOFFREY MAKOKHA (KNA)**

Kuunganisha wanaotoroka ukeketaji wa wanawake (FGM) na jamii kumetambuliwa kama mojawapo ya changamoto za wadau wa kupinga FGM kaunti ya Migori.

Wengi wa wasichana walio na umri wa kati ya miaka saba na 16 ambao wamekuwa wakihifadhiwa katika vituo kadhaa na maeneo salama hasa katika eneo la Kuria, wamekuwa na wakati mgumu kukubaliwa na jamii yao eneo hilo. Huku tarehe za kufungua shule zikikaribia haraka baada mwezi huu, wanaopiga vita ukeketaji wameanza mchakato wa kuhamasisha jamii kuhusu haja ya kukubali tena watoto wao. Afisa wa shirika lisilo la kiserikali, Tunaweza, Vincent Mwita anasema kwamba wasichana hao huwa wanamiminika katika vituo vya uokoaji na maeneo mengine salama kila Desemba kutoroka ukeketaji eneo la Kuria. Kufikia sasa, wasichana 312 wamejiunga na makao ya watoto naaeneo mengine salama msimu huu wa likizo ndefu ambavyo viko ndani ya kaunti ndogo mbili za Kuria.

Ingawa vita dhidi ya ukeketaji vimezidishwa katika miaka iliyopita, shida hiyo inaonekana kuathiri sana wanaopiga vita uovu huo.

Ukosefu wa chakula cha kutosha, maji safi na mahitaji mengine ya msingi kumekuwa tatizo kwa vituo vya muda vya uokoaji ambavyo huwa vinategemea misaada kutoka kwa wasamaria wema. Bw Mwita asema kwamba shida kubwa inayowakabili wanaopiga vita ukeketaji leo ni maridhiano na kuunganisha wasichana wanaookolewa na jamii. Wengi wa wasichana hao huwa wanatoroka bila kuwaeleza wazazi au walezi wao wakihofia kuzuiliwa nyumbani au kunyimwa nafasi na kulazimishwa kupashwa tohara.

ACA anti counterfeit authority
Promoting Genuine

**TANGAZO NAMBA . 4/2022**

**AWAMU YA KWANZA (1) YA UTEKELEZAJI WA REKODI ZA HAKIMILIKI ZA BIDHAA KWA UAGIZAJI**

Kando na Notisi yetu kwa Umma 3/2022 kuhusu utekelezaji wa Rekodi ya Uakili Haki za Mali na Kibali cha Kuagiza cha ACA ambacho kitaanza tarehe 1 Januari 2023, na kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Kupambana na Bidhaa Bandia Na. 13 ya 2008 (Kifungu cha 34B) na Kanuni za Kupambana na Bidhaa Bandia {Recordation} LN 118/2021 (R4) : Umma na wadau wanaarifiwa zaidi kuwa:
Mamlaka imechukua mbinu ya hatua kwa hatua ili kuwezesha kufuata mara kwa mara kwa waagizaji na wamiliki wa chapa. Bidhaa zilizo chini ya Kanuni zifuatazo za HS zimeainishwa chini ya Awamu ya Kwanza (1) ya mchakato wa utekelezaji na zitahitaji maombi ya kibali cha kuagiza cha ACA kuanzia Januari 1, 2023.

**Sura ya 85: Umeme na elektroniki Zenye Misimbo ya HS kutoka 8508 hadi 8544**

Orodha ya kina ya Kanuni za HS zinazodhibitiwa na ACA kulingana na Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Toleo la Kawaida la Ushuru wa Nje 2022 linapatikana kwenye tovuti ya ACA.

Kwa Utoaji wa Kibali cha Kuagiza cha ACA na usindikaji wa matamko ya chapa, tafadhali tembelea Mfumo wa Njia moja wa Kentrade kupitia ***tfp.kenyatradenet.go.ke.***. Kwa maelezo zaidi kuhusu Rekodi ya IPR na Kibali cha Kuagiza cha ACA, tembelea tovuti ya AIMS ya ACA katika **public.aims.aca.go.ke.**

Mpango wa Kurekodi wa IPR ni hatua ya kuwezesha biashara inayolenga kukuza biashara halali na ya haki nchini Kenya ingawa kukomesha uagizaji ghushi. Hii inalenga kulinda afya na usalama wa watumiaji na kuvutia uwekezaji.

Kwa habari zaidi, tembelea tovuti yetu kwa **www.aca.go.ke.** Barua Pepe: **recordation@aca.go.ke** au piga simu **+254202280000 /+254717430640.**

**Mkurugenzi MKuu**
**Mamlaka ya Kupambana na Bidhaa Bandia.**

KENYA VISION 2030

ELDOWAS
ELDORET WATER AND SANITATION COMPANY

The Nature Conservancy
Protecting nature. Preserving life.

**KAMPUNI YA MAJI NA USAFI YA ELDORET**
**P.O. BOX 8418-30100, ELDORET**
**Simu 053-2035000/200, B/Pepel:info@eldowas.or.ke**

**MRADI WA HAZINA MAJI ELDORET-ITEN NAFASI ZA KAZI**

Kampuni ya Maji na Usafi ya Eldoret (ELDOWAS) inatekeleza mradi wa miaka mitatu (3) unaofadhiliwa na GEF-IFAD, Eldoret-Iten Water Fund for Tropical Water Tower Conservation kwa ushirikiano na The Nature Conservancy ikijumuisha taasisi za umma na za kibinafsi. Mradi wa Hazina ya Maji wa Eldoret-Iten ni Ushirikiano wa Sekta ya Umma na Binafsi ambao unalenga kukuza usimamizi endelevu wa maliasili, kuimarisha mazingira wezeshi kwa mabadiliko katika sekta ya uzalishaji wa wakulima wadogo, na kupitisha fedha za maji kama nyenzo ya ufadhili endelevu wa shughuli za uhifadhi maeneo ya vyanzo vya maji yanayohudumia miji ya Eldoret na Iten.

Kampuni ya Maji na Usafi ya Eldoret, Mtoa Huduma ya Maji na Maji Taka, inakaribisha maombi kutoka kwa waombaji waliohitimu ipasavyo kujaza nafasi zifuatazo zilizoachwa wazi:

| | Jina la Kazi | Marejeleo | Idadi |
|---|---|---|---|
| 1. | Meneja wa Mradi | ELDOWAS/EIWF/2023/PM/01 | 1 |
| 2. | Mratibu wa Uhifadhi wa Shamba | ELDOWAS/EIWF/2023/FCC/02 | 1 |
| 3. | Afisa Ufuatiliaji na Tathmini/Usimamizi wa Maarifa | ELDOWAS/EIWF/2023/M&E,KMO/03 | 1 |
| 4. | Afisa wa Kusimamia Shughuli Tofauti | ELDOWAS/EIWF/2023/OPO/04 | 1 |
| 5. | Afisa wa Mifumo ya Taarifa za Kijiografia (GIS). | ELDOWAS/2023/GISO/01 | 1 |

Wagombeaji wanaopenda nafasi hizo wanatarajiwa kutimiza mahitaji ya uzoefu wa kina yaliyo katika tangazo kamili katika tovuti yetu **www.eldowas.or.ke** kujaza fomu ya maombi ya kazi na kuwasilisha tu kwa **jobs@eldowas.or.ke** mnamo au kabla ya tarehe **27 Januari 2023 saa 5.00 jioni.**
ELDOWAS ni mwajiri aliyejitolea kutoa nafasi kwa makundi yaliyotengwa, hivyo wanawake, watu wenye ulemavu na makundi yaliyotengwa wanahimizwa kutuma maombi.

Hakuna malipo yanayohitajika kwa hatua yoyote wakati wa mchakato wa kuajiri. Maombi ya wale watakaopatikana wakidanganya yatafutiliwa mbali. Tutawasiliana na wale watakaoorodheshwa pekee.

Wale waliofaulu wanapaswa kuwasilisha idhini kutoka kwa K**RA, HELB, EACC, CID - Cheti cha Maadili Bora na Mamlaka ya Kusimamia Ulipaji Mikopo.**

**Afisa Mkuu Mtendaji**
**Kampuni ya Maji na Usafi ya Eldoret**
**S.L.P 8418-30100 Eldoret**




“ Virusi havitembei, watu huvisambaza, tukiacha kutembea, virusi vitakufa”




# Serikali yatumia Sh1.7B kuunganisha stima katika nyumba 35,000 Nyeri

NA SAMUEL MAINA (KNA)

Kampuni ya stima ya serikali Kenya Power (KP) imetumia Sh1.7 bilioni kuunganisha stima katika nyumba 34,925 kaunti ya Nyeri chini ya mradi wa Last Mile tangu 2015. Ripoti ya meneja wa biashara KP katika kaunti hiyo Duncan Machuka inaonyesha kuwa shule za msingi 391 zimenufaika na mradi huo ambao umefadhiliwa pamoja na Serikali ya Kitaifa, Benki ya Dunia, Chama Cha Kimataifa cha Maendeleo na Benki ya Maendeleo Afrika. Kieni inaongoza ikiwa na nyumba

7,656 zilizowekwa stima ikifuatwa kwa karibu na Mathira ikiwa na nyumba 6,342, Tetu iikiwa na 5,949 na Mukurwe-ini ikiwa na nyumba 5,873.

Othaya na Nyeri Mjini ndizo zina idadi ya chini ya nyumba zilizowekwa stima katika orodha hiyo zikiwa na nyumba 4,778 na 4,327 mtawalia. Katika awamu ya kwanza ya mradi wa Last Mile, serikali ililenga nyumba 314,200 ikiwa ni Wakenya 1.5 milioni zaidi waliounganishiwa stima nchini.

Mradi huo ilikadiriwa kugharimu .

Sh13.5 bilioni na ulikuwa uhusishe kuwekwa kwa mtandao ulio na nguvu za chini kufikia nyumba zilizoko mita 600 kutoka iliko transfoma. Kampuni ya Kenya Power ilikuwa imetambua transfoma 5,320 zilizoko katika kaunti zote 47 kwa utekelezaji wa mradi huo katika awamu ya kwanza ambayo ilianza Septemba 2015. Ili kunufaika na mradi huo, wateja walitakiwa kulipa Sh15,000. Awamu ya pili na ya tatu ya mradi huo ilihusu kuwekwa kwa transfoma mpya na kuongeza mtandao wenye nguvu za chini kwa lengo la kufikia wateja wengine

500,000 zaidi, na hivyo basi, kuongeza Wakenya 2.5 walio na stima nyumbani.

Lengo la mradi huo lilikuwa ni kuunganisha stima asilimia 70 ya nyumba Kenya kufikia

2017 katika juhudi za kuafikia upatikanaji wa stima kwa wote kufikia 2020. Kwa wakati huu inakadiriwa kwamba asilimia 71 ya Wakenya wako na stima. Kwa jumula, serikali ilifaulu kuunganisha nyumba 176,363 kaunti ya Nyeri kati ya 248,873 ambazo zilituma maombi ya kuunganishiwa stima, ikiwa ni sawa na asilimia 70 ya uunganishaji wa stima. Wakati .huo huo, Machuka anasema kwamba kampuni hiyo inajitahidi kuhakikisha wateja wao wanahama kutoka mita za zamani za kulipia stima baada ya kutumia hadi mfumo wa kisasa wa kulipia mita.

Alisema kwamba kwa wakati huu, wateja, 3,000 tayari wanafurahia mita za kisasa na akaahidi kuongeza idadi hiyo wakipata shehena mpya ya vifaa hivyo. Na hili kutatua shida ya kukatika kwa stima kwa kila mara katika kaunti hiyo, afisa huyo alisema kampuni imetenga Sh

1.5 bilioni kuimarisha mtandao wake tangu mwaka wa 2013, mradi ambao utahusu kuongeza vituo zaidi katika kaunti ndogo zote nane.



REPUBLIC OF KENYA

## MINISTRY OF WATER, SANITATION AND IRRIGATION

### *STATE DEPARTMENT FOR WATER AND SANITATION*

### REQUEST FOR PROPOSAL (RFP)

### CONSULTANCY SERVICES FOR PUBLIC RELATION AND MEDIA OUTREACH FOR THE STATE DEPARTMENT FOR WATER AND SANITATION

### RFP NO.: SDWS/RFP/04/2022-2023

**1. Background**

The Ministry of Water, Sanitation and Irrigation through the newly created State Department for Water and Sanitation seeks to enhance and broaden its communication function with the sectors stakeholders by intensifying sharing information on its mandate within the Government. There is increased need for collaboration and sharing of the success stories on the many projects being undertaken by the Ministry as outlined in the Executive Order No. I of 2022 which sets the mandate as follows:

- Water Resources Management Policy and Standards;
- Water Catchment Area Conservation, Control and Protection;
- Water and Sewerage Services Management Policy;
- Waste Water Treatment and Disposal Policy;
- Water Quality and Pollution Control;
- Sanitation Management;
- Management of Public Water Schemes and Community Water Projects
- Water Harvesting and Storage for Domestic and Industrial Use
- Water Storage and Flood Control Management;

**The operationalization of the mandate is hinged on the following legal instruments which need to be explained to the public and relevant sector stakeholders:**

- Water Act 2016
- Sessional Paper No. 1 of the National Water Policy 2021
- KEWI Act 2001
- Hydrologists Act 2017
- Legal Notice No. 252 of 18th December, 2015
- Relevant Strategies
- Guiding Regulations

**2. Objectives of the PR Consultancy**

To support Public Relations & Media outreach work and ensure the visibility of the projects under its mandate, the State Department for Water and Sanitation intends to engage the services of a duly registered Public Relations and Media Consultancy firm not only qualified and experienced in publicity, but competent in Developing Communication Strategies, Communication Plans and conveying in an appropriate fashion to local and international media outlets.

**Objectives of the assignment**

The objective of the assignment is to:

a) Provide requisite analytical support to the State Department for Water and Sanitation to understand the relevant stakeholder expectations, geographical mix along with positioning strategies and provision of highlights of the projects under implementation

b) Translate the above analysis into an effective communications and engagement strategy for the State Department, targeted at beneficiaries and the end users of its services. The engagement strategies would be detailed and operationalised in the form of brochures, newsletters, top quality presentations, presentation templates, information memorandums, et al. to help SDW&S communicate effectively to the public(s).

**3. Scope Works and Deliverables**

The scope of publicity initiatives will be focused on the following areas of the State Department for Water and Sanitation's mandate which include:

- Water Resources Management Policy and Standards;
- Water Catchment Area Conservation, Control and Protection;
- Water and Sewerage Services Management Policy;
- Waste Water Treatment and Disposal Policy;
- Water Quality and Pollution Control;
- Sanitation Management;
- Management of Public Water Schemes and Community Water Projects
- Water Harvesting and Storage for Domestic and Industrial Use
- Water Storage and Flood Control Management;

**The scope will specifically include:**

- Event organization
- Branding and packaging of Ministry's projects and programs
- Production of documentaries
- Liaison with media houses
- Liaising with the management and the Deputy Director of Public Communications to identify suitable topics to produce news items, material for the website, print and electronic media, to enhance the visibility of the SDWS in implementation of its mandate both locally and internationally.
- Working with the State Department for Water and Sanitation to support the preparation of press releases, speeches, and other communications products which will be identified within the period of the consultancy.
- Ensuring that important Ministry's functions are well covered in the media by making appropriate media invites and interventions.
- Providing advice and technical support during showcasing, innovation and branding events of the State Department for Water and Sanitation
- Tracking, monitoring and reporting on new developments, best practices in Water and Sanitation sector management on related and relevant national and international events to promote peerage and knowledge transfer.
- Identifying opportunities for linkages for further public relations work around the themes of Water and Sanitation with the like-minded stakeholders in both public and private entities.

4. Interested consulting firms **MUST** provide among others the following certified documents:
   1. Company Profile
   2. Certificate of Registration/Incorporation
   3. Current CR 12
   4. Valid Tax Compliance Certificate
   5. Latest 3 years audited financial statements (2022, 2021 and 2020)
   6. Power of Attorney
   7. Valid Business Permit
   5. Firms may associate with other firms in the form of joint venture or sub-consultancy to enhance their qualifications.

6. The completed RFP documents, in one (1) original and a copy properly paginated must be delivered to the Tender Box on Ground Floor, Maji House or sent to the address below so as to be received on or before 11th February, 2023 at 10.00 am East African time. Bulky tender documents should be registered in Room 322 Maji House, Nairobi, Ministry of Water, Sanitation and irrigation Headquarters during normal working hours.

7. The RFP documents deposited at the Tender Box should be clearly marked:

**RFP NO.: SDWS/RFP/04/2022-2023**
**"CONSULTANCY SERVICES FOR PUBLIC RELATION AND MEDIA OUTREACH FOR THE STATE DEPARTMENT FOR WATER AND SANITATION"**
and addressed to:
**The Principal Secretary**
**State Department for Water and Sanitation**
**Maji House, 3rd Floor, Room 322, Ngong Road**
**P. O. Box 49720-00100, Nairobi**
**Tel: +254 02 2716103 Ext. 42224**
**Email: pswater.go.ke , www.water.go.ke**

8. Tendering will be conducted through the Quality and Cost Based Selection (QCBS) procedures specified in the Procurement Laws of Kenya, and is open to all eligible bidders as defined in the tender Documents.

9. Tenders will be opened immediately thereafter, in the presence of bidders or representatives who choose to attend and sign a record of attendance.

10. A complete set of Bidding Documents in English language may download free of charge from the Ministry's Website **http://www.water.go.ke** or Public Procurement Information Portal. **https://www.tender.go.ke**.

**Signed**
**Principal Secretary, State Department for Water and Sanitation**

## KENYATTA NATIONAL HOSPITAL

### PUBLIC NOTICE

### DISPOSAL OF UNCLAIMED BODIES

Kenyatta National Hospital is in its possession a number of unclaimed bodies at its Farewell Home. Pursuant to **Public Health Act Cap 242 [Subsidiary Legislation PUBLIC HEALTH (PUBLIC MORTUARIES) RULES,1991]**, interested members of the public are therefore requested to identify and collect the bodies within **7 days**, failure to which the hospital will seek authority from the courts to dispose them. The list of the bodies is available at the KNH Farewell Home and can also be accessed on the link below:

**www.knh.or.ke or https://knh.or.ke/index.php/disposal-of-unclaimed-bodies/**

**KNH FAREWELL HOME**

Funika mdomo unapopiga chafya
Nawa mikono na sabuni/ Sanitaiza
Jitenge na walio na virusi
Usiguse macho, pua au mdomo na mikono michafu
Pika nyama na mayai ziive. Usile chakula kibichi
Hakikisha maeneo yote ni safi
KOMESHA COVID-19



KBC
YOUR NATIONAL BROADCASTER

## NOTISI YA TENDA

Kenya Broadcasting Corporation inaalika wanaopenda kushiriki kwenye tenda kutuma maombi yafuatayo:

| | |
|---|---|
| **TENDER NO.9/KBC/2022-23** | **UTOAJI WA HUDUMA ZA ULINZI KATIKA VITUO VYA DIJITALI** |

Stakabadhi kamili za tenda zinaweza kuchukuliwa na wanaotaka kutuma maombi kwenye mtandao wa shirika , **www.kbc.co.ke, tenders.go.ke(PPIP)** au kuchukua nakala kamili kutoka kwa **afisi ya Meneja wa Ununuzi** katika Broadcasting House Harry Thuku Road. Wanaopenda kushiriki kwenye tenda hii wanahitajika kujiandikisha kwa kulipa Sh1.000 ambazo hazirudishwi pesa taslimu au hundi ya benki kwa keshia wa Kenya Broadcasting Corporation kwenye barabara ya Harry Thuku Road kabla ya tarehe ya mwisho ya kurudisha stakabadhi za tenda. (Vijana, wanawake na walevamu) hawahitaji kulipa Sh1000. Pia wanaochukua stakabadhi kutoka kwenye tovuti hawahitajiki kulipa lakini papo hapo wawasilishe maelezo yao ili kusajiliwa na kwa lengo la kupokea ufafanuzi zaidi kuhusu tenda na maelezo zaidi kwa afisi ya ununuzi ya KBC au **procurement@kbc.co.ke**.

Tenda zilizojazwa zinapasa kuwasilishwa kwenye bahasha iliyofungwa na kuandikwa nambari ya tenda na kutumwa kwa:-

**Mkurugenzi Mkuu,**
**Kenya Broadcasting Corporation,**
**S.L.P 30456-00100, NAIROBI**

**au**

Kuwekwa ndani ya sanduku la tenda katika lango kuu Broadcasting House mnamo au kabla ya **Januari 24, 2023** saa **4.00 asubuhi.** Maombi yaliyotumwa yatafunguliwa mara moja katika afisi ya KBC Matangazo mbele ya waliotuma maombi au wawakilishi wao watakaoamua kuhudhuria.

**MKURUGENZI MKUU**

KENYA VISION 2030

**KENYA PLANT HEALTH INSPECTORATE SERVICE (KEPHIS)**

## NOTISI YA TENDA

Kenya Plant Health Inspectorate Service (KEPHIS) ni shirika la kiserikali ambalo wajibu wake mkuu ni kihakikisha pembejeo za kilimo na mazao ni za hali ya juu ili kuzuia athari mbaya kwa uchumi wa nchi, mazingira na afya ya binadamu. KEPHIS ingependa kutoa mwaliko wa maombi kwa tenda zifuatazo:

| Nambari ya tenda | Jina la Tendae | Tarehe ya kufungwa |
|---|---|---|
| K/T/7/2022-2023 | Tenda ya kununua, kuweka na kuzindua huduma za intaneti katika Makao Makuu ya KEPHIS na afisi za maeneo ; K/T/07/2022-2023; ***(Tenda Wazi ya Kitaifa)*** | Januari 30, 2023 saa 4:30 asubuhi. |
| K/T/8/2022-2023 | Tenda ya utoaji wa mitambo ya kuhifadhi data; K/T/08/2022/2023. ***(Tenda Wazi ya Kitaifa - (Marudio)*** | Januari 30, 2023 saa 4:30 asubuhi. |
| K/T/9/2022/2023 | Tender for disposal of boarded motor vehicles. ***(Open National Tender).*** | 30th January 2023 10:30 am. |

Kwa maelezo zaidi, ukaguzi na kudondoa stakabadhi za tenda, tafadhali tembelea tovuti yetu: **www.kephis.org** au **www.tenders.go.ke.**

**MKURUGENZI MKUU**
**KENYA PLANT HEALTH INSPECTORATE SERVICE**

KENYA VISION 2030

REPUBLIC OF KENYA
Kenya Power

## MAOMBI YA TENDA

Kenya Power inaalika maombi ya tenda kutoa huduma zifuatazo:-

| NO. | NAMBARI YA TENDA | MAELEZO YA HUDUMA | TAREHE YA KUANZA TENDA | MKUTANO/ KUTEMBELEA ENEO | TAREHE YA MWISHO |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | KP9/9A/OT/ HRA/03/22-23 | Kukarabati makazi ya wafanyakazi ya Ondiek | Jumanne 10.01.2023 | Jumanne 17.01.2023 saa 4.00 asubuhi **(Demonstration Centre, Electricity House, Kisumu)** | Jumanne 24.01.2023 saa 4.00 asubuhi. |
| 2. | KP1/9A.2/OT/ 017/NW/22-23 | Kununua, kuweka na kukarabati mitambo ya kusafisha hewa katika vituo vyetu vidogo | Jumatano 11.01.2023 | Jumanne 17.01.2023 saa 3.00 asubuhi. **(Stima Plaza Auditorium, Kolobot Rd, Parklands, Nairobi)** | Alhamisi 02.02.2023 saa 4.00 asubuhi. |
| 3. | KP1/9A.2/OT/ 015/SEC/22-23 | Makubaliano ya miaka miwili (SLA) kukarabati mitambo ya kutoa tahadhari kuhusu moto katika Electricity House, Nairobi | Jumatano 11.01.2023 | Alhamisi 19.01.2023 saa 4.00 asubuhi. **(Stima Plaza Auditorium, Kolobot Rd, Parklands, Nairobi)** | Jumatano 01.02.2023 saa 4.00 asubuhi |
| 4. | KP1/9A.2/OT/ 023/ICT/22-23 | Makubaliano ya kukarabati (SLA) na kutunza mitambo ya UPS katika afisi za maeneo za KPLC, Depo na Matawi | Alhamisi 12.01.2023 | N/A | Jumatano 01.02.2023 saa 4.00 asubuhi. |
| 5. | KP1/9A.2/OT/ 006/22-23 | Utoaji huduma za kitaaluma za mipango | Jumatano 11.01.2023 | N/A | Alhamisi 02.02.2023 saa 5.00 asubuhi. |

Hati za tenda zinazotoa maelezo kamili kuhusu tenda zilizotajwa hapo juu zinaweza kupatikana kutoka mtandao wa Kenya Power (**www.kplc.co.ke**) kuanzia tarehe zilizotajwa juu.

**GENERAL MANAGER**
**SUPPLY CHAIN & LOGISTICS**

**www.kplc.co.ke**

DIAL *977# | Access Kenya Power services fast and easy

REPUBLIC OF KENYA

## WIZARA YA KAWI NA MAFUTA

## IDARA YA KAWI

## TANGAZO LA ZABUNI

Wizara ya Kawi na Mafuta, Idara ya Mafuta inakaribisha zabuni kutoka kwa kampuni zinazostahiki kwa zabuni ifuatayo;

| Namba ya Zabuni | Maelezo | Uhitimu | Kufunga na Wakati |
|---|---|---|---|
| MOEP/SDE/ONT/01/2022-2023 | Ujenzi, Upimaji, Uagizaji wa Mitambo ya Kitaasisi ya Uashi ya 60m3 ya Biogas Kwa Kutumia Kinyesi Ng'ombe | Wazi kwa wote | Wednesday, 25th January 2023 at 10.00 am |

Wazabuni waliohitimu na wanaovutiwa wanaweza kupata maelezo zaidi na kukagua hati za Zabuni wakati wa saa za kazi (0900 hadi 1700) kwenye anwani iliyo hapa chini.

Wazabuni wanaohitajika wanaweza kuomba ufafanuzi kuhusu Zabuni hadi siku Nne (4) kabla ya tarehe ya kuwasilisha Zabuni. Ombi lolote la ufafanuzi lazima liandikwe kwa maandishi na kushughulikiwa kwa:

**Katibu wa Wizara**
**Wizara ya Kawi na Mafuta**
**Idara ya Kawi**
**P.O. Box 30582-00100**
**Nairobi, Kenya**
**Simu:+254-20-310112**
**Barua pepe:supplychain@energy.go.ke**

Seti kamili ya hati za zabuni zilizo na vigezo vya kina vya kufuzu zinaweza kununuliwa au kupatikana na wazabuni walio na nia kutoka kwa ofisi ya Usimamizi waMfumo wa Usambazaji kwenye Orofa ya 1, Kawi Complex Block 'A' baada ya malipo ya ada isiyorejeshwa ya shilingi elfu moja kwa taslimu au Hundi ya Benki na kulipwa kwa Katibu Mkuu, Wizara ya Kawi na Mafuta, Idara ya Kawi. Nyaraka za zabuni zinaweza pia kupatikana kielektroniki kutoka kwa Tovuti www.energy.go.ke na www.tenders.go.ke ***bila malipo***. Wale wanaopata hati zao za zabuni kwa njia ya kielektroniki wanaombwa kuwasilisha maelezo ya jina la kampuni, anwani ya posta na ya mahali, barua pepe na nambari za simu za mawasiliano kwa madhumuni ya kuwasilisha ufafanuzi wowote na/au nyongeza kwenye hati za Zabuni.

Nyaraka za zabuni zilizokamilishwa zilizoambatanishwa katika bahasha zilizofungwa na kuwekewa alama ya jina la zabuni na nambari ya kumbukumbu zinapaswa kutumwa kwa:

**Katibu Mkuu**
**Wizara ya Kawi na Mafuta**
**Idara ya Kawi**
**Kawi Complex Block 'A', South C**
**Popo Lane, Nje ya Barabara ya Red Cross**
**P.O Box 30582-00100**
**Nairobi**

Na itawekwa kwenye Sanduku la Zabuni lililo kwenye lango la kuingilia, Orofa ya Chini, Kawi Complex Block 'A' ili ipokewe kabla au **25 Januari, 2023** saa **10.00 asubuhi.**

Nyaraka za Zabuni zitafunguliwa mara moja katika chumba cha mikutano katika orofa ya 3 ya Kawi Complex Block 'A' mbele ya wagombea au wawakilishi wao wanaochagua kuhudhuria.

Zabuni zilizochelewa zitakataliwa na kurejeshwa bila kufunguliwa.

**Mkuu, Huduma za Mfumo wa Usambazaji**
**KWA: KATIBU MKUU**

KENYA VISION 2030

“ Virusi havitembei, watu huvisambaza, tukiacha kutembea, virusi vitakufa”




# Mpango mpya wa KRA kusaidia kupitisha bidhaa haraka nchini

**NA EDNA OKOTH (KNA)**

Mamlaka ya Ukusanyaji Ushuru Kenya (KRA) imepatoa Wahudumu wa Uchumi Walioidhinishwa 300 (AEOs) Vyeti vya Kuwatambua ili kuinua usafirishaji na uondoaji wa bidhaa katika vituo vyote vya kuingia nchini. Kamishna wa Forodha na Uthibiti wa Mipaka wa KRA BiLilian Nyawanda alisema kwamba vyeti hivyo vilivyotolewa na Mamlaka hiyo kwa AEOs 300, vitawezesha waagizaji na wauzaji bidhaa nje ya nchi kutambuliwa kwa urahisi.

Bi Nyawanda alisema kwamba kutambuliwa kwa AEOs pia kutasaidiav kupunguza muda wa kuondoa mizigo na gharama inayohusiana na uagizaji na uuzaji wa bidhaa nje ya nchi na kuhakikisha biashara salama, na halali nchini.

“KRA imejitolea kuwezesha uharakishaji wa mchakato wa kushughulikia mizigo ya kampuni zinazodumisha viwango vya juu vya uzingatiaji kwa kuwa zinashiriki biashara halali,” alisema Nyawanda na kuongeza kuwa takriban asilimia 30 ya mapato ya forodha yanakusanywa kutoka kwa AEO walioidhinishwa kuuza bidhaa nje ya nchi.

Alitangaza kuwa mamlaka hiyo inatazamia kuongeza kiwango hicho kwa kuimarisha uwezeshaji wa biashara kwa AEOs waliopo huku ikipanua mpango huo kujumuisha wanaolipa ushuru katika vipengee vingine kama vile wenye mabohari na biashara za kati.

Kamishna huyo wa forodha alikuwa akizungumza katika hafla ya kufunguliwa kwa Wahudumu wa Uchumi Walioidhinishwa iliyoandaliwa na Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ) kwa ushirikiano na KRA katika hoteli moja ya Nairobi.

Mpango huo wa AEOs unalenga kuimarisha taratibu za kuwezesha biashara kupitia kuharakisha uondoaji wa mizigo na kurahisisha michakato ya uagizaji na uuzaji bidhaa nje ya nchi.

Wakati wa hafla hiyo, kampuni zilizoidhinishwa kama AEO zilipatiwa vyeti vya kuzitambua kama sehemu ya kuimarisha michakato ya uagizaji na uuzaji wa nje ya nchi na kuinua biashara.

Nyawanda alihimiza wafanyabiashara ambao kwa wakati huu wako katika mpango wa AEO kuwa mabalozi wema kwa kuhimiza ulipaji wa ushuru na kusaidia kuondoa wasiolipa ushuru katika biashara.

---

REPUBLIC OF KENYA

## WIZARA YA MASUALA YA VIJANA, MICHEZO, NA SANAA

### IDARA YA MASUALA YA VIJANA

## MAOMBI YA ZABUNI
## HUDUMA ZA USHAURI -KUTEUA MASHIRIKA

| | |
|---|---|
| **Nchi** | **KENYA** |
| **Jina la Mradi** | **Mradi wa Ajira na Fursa za Vijana wa Kenya** |
| **Nambari ya Mkopo/Ruzuku** | **5812-KE** |
| **Kichwa cha Kazi** | **Huduma za Ushauri kwa Mafunzo ya Wafuatiliaji Walengwa (Kazi ya 3** |
| **Nambari ya Marejeleo** | **KE-MPYG-321438-CS-QCBS** |

Serikali ya Kenya imepokea ufadhili kutoka kwa Benki ya Dunia kugharamia Mradi wa Ajira na Fursa kwa Vijana wa Kenya na inakusudia kutumia sehemu ya mapato ya Ununuzi wa Huduma za Ushauri. Mradi unalenga vijana wa kiume na wa kike wasio na ajira wenye umri wa miaka 18-29 na wasiozidi elimu ya sekondari ambao hawana ajira au wanaofanya kazi katika mazingira magumu. Mradi huu unatekelezwa katika mkabala wa kipengele unaojumuisha 1) kuboresha uwezo wa kuajiriwa 2) usaidizi wa kubuni nafasi za kazi, 3) kuboresha taarifa za soko la ajira na, 4) kuimarisha maendeleo ya sera ya vijana na usimamizi wa miradi.

KYEOP inatekelezwa kwa pamoja na Wizara ya Masuala ya Vijana, Michezo, na Mamlaka ya Sanaa, Biashara Ndogo na Biashara Ndogo (MSEA), Mamlaka ya Kitaifa ya Mafunzo ya Viwanda (NITA) na Wizara ya Kazi na Ulinzi wa Jamii (MLSP). Huduma za ushauri (“Huduma”) ni pamoja na Kuendesha Mafunzo ya Wafuatiliaji kwa vipengele viwili vya kwanza vinavyoshughulikia kipindi cha Juni, 2020 hadi Desemba, 2023. Kipengele cha kwanza, kinachohusu kuboresha uajiri, kinatekelezwa kwa pamoja na Wizara ya Masuala ya Vijana, Michezo na Sanaa na NITA. Kipengele hiki kinawapa vijana walengwa mafunzo na uzoefu wa kazi katika sekta binafsi au mafundi mahiri kwa lengo la kuboresha matokeo ya ajira kwa vijana. Kipengele cha pili, ambacho kinajumuisha usaidizi wa uundaji wa ajira, kinatekelezwa kwa pamoja na MSEA na Wizara ya Masuala ya Vijana, Michezo na Sanaa. Ili kutathmini ufanisi wa mapato ya KYEOP, itakuwa muhimu kuwafuatilia wahitimu ili kupima matokeo ya Mradi katika suala la ajira, mapato, uboreshaji wa ujuzi, manufaa ya ujuzi waliopata, changamoto zinazowakabili wahitimu na matokeo ya mafunzo yote yanayotolewa na KYEOP. Masomo ya Tracer pia yatashughulikia vijana wanufaika ambao hawakuhitimu na walioacha shule ili kueleweа vyema sababu za kutokamilika kwa programu
Wizara ya Masuala ya Vijana, Michezo na Sanaa sasa inakaribisha Mashirika ya Ushauri yanayostahiki (***“Washauri”)*** ili kuonyesha nia yao ya kutoa Huduma. Washauri Wanaovutiwa wanapaswa kutoa habari inayoonyesha kuwa wana sifa zinazohitajika na uzoefu unaofaa kutekeleza Huduma.

Vigezo vya uteuzi ni:
1) Kiwango cha chini cha uzoefu wa miaka mitano muhimu na uwezo wa kiufundi katika utekelezaji wa tafiti za ufuatiliaji (2017 hadi sasa).
2) Angalau kazi mbili za asili zinazofanana katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2017 hadi sasa), moja wapo inapaswa kuwa katika elimu au ajira.
3) Uzoefu katika kufanya tathmini za walengwa (toa taarifa za kuunga mkono kutoka kwa uzoefu uliopita).
4) Onyesho la uwezo wa kuchambua data kwa ukali na kuwasilisha matokeo kwa hadhira isiyo ya kiufundi.

Wataalamu Muhimu hawatatathminiwa katika hatua ya kuorodhesha.
Uangalifu wa Washauri wanaovutiwa umetolewa kwenye aya ya 1.9 ya Miongozo ya Benki ya Dunia: Uteuzi na Ajira ya Washauri [chini ya Mikopo ya IBRD na Mikopo ya IDA & Ruzuku] na Wakopaji wa Benki ya Dunia, Januari 2011 Iliyorekebishwa Julai 2014 ***(“Mwongozo wa Mshauri”***), ikiwekwa wazi. sera ya Benki ya Dunia juu ya mgongano wa maslahi. Zaidi ya hayo, tafadhali rejelea maelezo mahususi yafuatayo kuhusu mgongano wa kimaslahi kuhusiana na kazi hii: 1.9 (b) ya Miongozo ya Mshauri.

Washauri wanaweza kushirikiana na makampuni mengine ili kuboresha sifa zao lakini wanapaswa kuonyesha wazi kama chama kiko katika mfumo wa ubia na/au ushauri mdogo. Katika kesi ya ubia, washirika wote wa ubia watawajibika kwa pamoja na kwa kiasi kikubwa kwa mkataba mzima ikiwa watachaguliwa. Walakini, uzoefu wa mshauri mdogo hautazingatiwa wakati wa kuorodhesha fupi. Mshauri atachaguliwa kwa mujibu wa Mbinu ya Uteuzi wa

Ubora na Gharama iliyowekwa katika Miongozo ya Mshauri ya Benki ya Dunia inayotumika: Uteuzi Ajira ya Washauri Waombaji wanaostahiki wanaovutiwa wanaweza kupata maelezo zaidi kutoka kwa **Ofisi ya Usimamizi wa Usambazaji, Orofa ya 3, Chumba Namba 321 katika ofisi za KYEOP, Bruce House, Standard Street,** wakati wa saa rasmi za kazi (saa 8.00 asubuhi -5.00 jioni.). Jaza hati ya REOI (iliyopigwa rangi na kupigwa mhuri/kutiwa saini kwenye kila ukurasa) na kuambatanishwa katika bahasha iliyotiwa muhuri wazi iliyo na nambari ya marejeleo ya zabuni na kutumwa kwa Katibu, Idara ya Masuala ya Vijana P. O. Box 30050 - 00100, Nairobi, Kenya inapaswa kuwekwa ndani ya Sanduku la Zabuni katika Orofa ya 3 ya Bruce House litakalopokelewa mnamo au kabla ya **Jumanne, 24 Januari 2023** saa **10.00** asubuhi

REOI zitafunguliwa mara baada ya hapo mbele ya watahiniwa au wawakilishi wao katika Ukumbi wa Bodi ya KYEOP, Bruce House, Orofa ya 3 Barabara ya Standard Nairobi.

**KATIBU**
**IDARA YA MASUALA YA VIJANA**

KENYA VISION 2030

REPUBLIC OF KENYA

## KENYA PIPELINE COMPANY LIMITED

***Africa's Premier Oil & Gas Company***

KENPIPE PLAZA,
SEKONDI ROAD,
OFF NANYUKI ROAD,
INDUSTRIAL AREA,
NAIROBI, KENYA.
P.O.Box 73442 - 00200,
TELEPHONE: 254-20-2606500-4
MOBILE: 0722 207 678/9
0734 333 217/219/234/226
E-mail: Info@kpc.co.ke

## MWALIKO WA ZABUNI

Kampuni ya Kenya Pipeline Ltd inaalika zabuni zilizofumwa kutoka kwa wawaniaji wanaofuzu ifuatavyo:

| NA. | MAREJELEO & MAELEZO YA ZABUNI | DHAMANA YA ZABUNI | ZIARA YA ENEO | TAREHE YA MWISHO |
|---|---|---|---|---|
| | **ZABUNI WAZI YA KITAIFA** | | | |
| 1. | **KPC/PU/OT-193/SEC/NBI/22-23**<br>Utoaji wa Huduma za Usalama kwa Kipindi cha Miaka Miwili - 1 Mei 2023 hadi 30 Aprili 2025 | Kes.200,000.00 | N/A | 01-02-2023 |
| | **FRAMEWORK CONTRACTS** | | | |
| 2. | **KPC/PU/OT-194/QC/NBI/22-23**<br>Zabuni ya Mkataba wa Mwongozo wa Utoaji wa Huduma za Wakala wa Usafirishaji wa Sampuli za Petroli za PTP kwa muda wa miaka 2. | N/A | N/A | 02-02-2023 |
| 3. | **KPC/PU/OT-195/QC/NBI/22-23**<br>Zabuni ya Mkataba wa Mwongozo wa Matengenezo ya Mara kwa Mara na Marekebisho ya Vifaa vya Maabara kwa muda wa miaka 2 | N/A | N/A | 02-02-2023 |
| | **RE - TENDER** | | | |
| 4. | **KPC/PU/OT – 156/KPRL/NBI/22 - 23**<br>Zabuni ya Usambazaji wa Vifaa kwa ajili ya Kukamilisha eneo la Upakiaji kwenye Malori la PS15 | Kes.200,000.00 | N/A | 03-02-2023 |
| 5. | **KPC/PU/OT – 106/WELFARE/NBI/22 - 23**<br>Zabuni ya Usambazaji wa Sare wa Wafanyakazi | Kes.100,000.00 | Utazamaji wa sampuli ni kati ya 19-01-2023 kuanzia saa 9.00a.m. hadi 1.00p.m. na 2.00p.m. hadi 3.00p.m asubuhi. | 03-02-2023 |

Nakala za Zabuni zinaweza kutazamwa na kupakuliwa kutoka kwa tovuti www.kpc.co.ke bila gharama yoyote. Wazabuni wanahitajika kusajili kampuni zao kwenye tovuti ya KPC SRM na kutuma maswali **PEKEE** kwa opentender@kpc.co.ke. Aidha, nyongeza zote zitabandikwa kwa mafaa ya wazabuni hao ambao wanaonyesha nia yao ya kushiriki kupitia tovuti ya SRM.

Hakuna anwani nyingine za barua-pepe zitakazotumika wala KPC haitawajibika ikiwa wazabuni wataamua kutuma hoja zao kwa anwani nyingine za barua pepe.

**FAHAMU: Wazabuni ambao hawajasajiliwa katika Mfumo wa KPC SRM wanapaswa kujisajili kwanza kwa kutumia kiungo hiki https://e-procurement.kpc.co.ke/irj/portal**

Mafunzo na miongozo ya zabuni hii inapatikana kwenye tovuti ya KPC www.kpc.co.ke/Tenders - Miongozo ya Mtumiaji ya SRM

Wazabuni wote watahitajika kuwasilisha zabuni hizo mtandaoni kupitia Tovuti ya SRM https://e-procurement.kpc.co.ke/irj/portal na ni **SHARTI** nakala zote zipakiwe kwenye **COLLABORATION FOLDER**. Wazabuni wasiambatanishe nakala zao kwenye kichupo kingine chochote cha tovuti. Nakala hizo zitapokelewa mnamo au kabla ya tarehe iya kufunga saa nne kamili asubuhi.

**(HAKUNA ZABUNI ZITAKUBALIWA KWENYE SANDUKU LA ZABUNI IWAPO HAZITAKUWA NA DHAMANA HALISI YA ZABUNI)** Ufunguzi wa zabuni utafanyika **saa nne unusu asubuhi.**

**KAIMU MENEJA MKUU (KITENGO CHA UNUNUZI)**
**FOR: MANAGING DIRECTOR**

KENYA VISION 2030

*INVITATION TO TENDER*

REPUBLIC OF KENYA

KenGen
Kenya Electricity Generating Company PLC

## MWALIKO WA ZABUNI

| NA | NA. YA ZABUNI | MAELEZO | UHITIMU | TAREHE YA MWISHO |
|---|---|---|---|---|
| 1 | KGN-IT-01-2023 | Zabuni ya Usambazaji, Uwasilishaji, Ukarabati na Utunzaji wa Kompyuta na Laptopu Maalum na Vipuri vyake. | Wakandarasi raia | 23 Januari 2023 saa10.00am |
| 2 | KGN-GDD-02-2023 | Zabuni ya Usambazaji wa huduma za Uboreshaji na utumiaji wa maombi ya Leseni mpya za Programu mbalimbali za Ziada za Uhandisi. | Wakandarasi raia | 23 Januari 2023 saa10.00am |
| 3 | KGN-GDD-03-2023 | Zabuni ya Usambazaji wa viunganishi vya Mitambo ya Pampu ya Hotwell (Pampu za Mitungi) ya Viwanda vya Umeme wa Wellhead. | Wakandari raia | 24 Januari 2023 saa 2.00pm |
| 4 | KGN-REG-01-2023 | Zabuni ya Ukarabati wa Chemchemi ya Eburu ya Maji Msituni ya 7HA (Awamu ya II) - Kaunti ya Nakuru<br><br>***Kutakuwa na ziara ya lazima ya eneo husika tarehe 17 Januari 2023 katika eneo la Eburru - Kaunti ya Nakuru kuanzia saa nne kamili asubuhi.*** | Wanawake | 26 Januari 2023 saa 2.00pm |
| 5 | KGN-BDD-01-2023 | Ombi la Mapendekezo (RFP) ya kutoa Huduma za Ushauri wa Utafiti wa Uwezekano Yakinifu wa Upanuzi wa Kiwanda cha Umeme cha Olkaria II<br><br>***Kutakuwa na ziara ya lazima katika eneo tarehe 24 Januari 2023 kuanzia saa nne kamili asubuhi; mkutano utakuwa Geothermal Plaza - Olkaria kabla ya kuelekea katika eneo.*** | Wazi Kimataifa | 7 Februari 2023 saa 10.00am |

Kampuni zinazovutiwa zinaweza kupata maelezo zaidi kutoka kwa afisi ya Meneja Mkuu, Kitengo cha Ununuzi, Simu: **(254) (020) 3666230**, Barua-pepe: **tenders@kengen.co.ke** katika siku za kawaida za kazi kuanzia tarehe ya kuchapishwa kwa tangazo hili. Nakala za zabuni zinaweza kuchukuliwa baada ya malipo ya ada isiyorejeshwa ya KSh.1, 000.00 inayofaa kulipwa kwa pesa taslimu au kwa hundi ya benki katika ofisi yoyote ya fedha ya KenGen.

Nakala hiyo pia inaweza kutazamwa na kupakuliwa kutoka kwa tovuti **www.kengen.co.ke** na katika tovuti ya Ununuzi wa kielektroniki **https://eprocurement.kengen.co.ke:50001/irj/portal.**

***Wazabuni wanashauriwa kutembelea tovuti na katika mtandao wa ununuzi wa kielektroniki mara kwa mara kwa maelezo yoyote ya ziada /ufafanuzi/nyongeza. Nakala zilizopakuliwa ni BURE. .***

### KUWASILISHA ZABUNI:

1. Nakala za zabuni lazima ziwasilishwe mtandaoni kupitia tovuti ya KenGen E-Procurement inayopatikana kwenye tovuti ya KenGen (**www.kengen.co.ke**)
2. Wazabuni wanaovutiwa na zabuni hii **SHARTI** wahakikishe kuwa wamesajiliwa katika Tovuti ya Ununuzi wa Kielektroniki. Tafadhali hakikisha unazingatia yafuatayo;
   - Kwa wasambazaji wanaojisajili kwa mara ya kwanza wahakikishe wametia alama kwenye kisanduku cha ***"Public Procurement"*** ili maelezo ya kuingia yatumwe kwa wasambazaji wahusika kiotomatiki.
   - Sharti hati zote zipakiwe kwenye Mfumo wa SRM kupitia kwa **https://eprocurement.kengen.co.ke:50001/irj/portal** inapatikana katika **www.kengen.co.ke**
   - Bei zitakazowekwa chini ya kipengee cha RFx zinafaa ziwe sawa na bei katika ratiba ya bei.

**Kumbuka;** Wazabuni wanaowasilisha zabuni zao na wanaotaka kuzirekebisha zaidi hawapaswi kubofya **WITHDRAW** bali bonyeza **EDIT** ili kuwawezesha kurekebisha majibu yao ya zabuni na kufanya mabadiliko yanayofaa.
Wazabuni wanaohitaji usaidizi wa aina yoyote kuhusu jinsi ya kupata zabuni kupitia mfumo huu wanashauriwa kupakua mwongozo kutoka kwa tovuti au wanaweza kuwasiliana nasi kupitia **eprocurement@kengen.co.ke**

**Dhamana Halisi ya Zabuni** pale inapohitajika katika fomu na kiasi kilichobainishwa sharti ziwasilishwe kwenye bahasha iliyofumwa vizuri na kuandikwa nambari ya zabuni na maelezo ya zabuni kabla ya tarehe ya mwisho kwa anwani ifuatayo:

**General Manager- Supply Chain,**
**Kenya Electricity Generating Company PLC,**
**9th Floor, KenGen Pension Plaza II,**
**Kolobot Road, Parklands,**
**P.O. Box 47936, 00100**
**NAIROBI**

Zabuni zitafunguliwa **mtandaoni** punde tu baada ya muda wa kufunga mbele ya wawakilishi wa wawaniaji watakaoamua kuhudhuria katika KenGen Pension Plaza II, chumba cha ufunguzi wa Zabuni, orofa ya 6.

***FAHAMU: KenGen inazingatia viwango vya juu vya uadilifu katika shughuli zake za biashara. Ripoti tabia yoyote isiyo ya kimaadili mara moja kwa njia hizi za mawasiliano zisizotambua jina la mhusika.***

1) **Piga bila malipo: 0800722626**
2) **Faksi: 00800 007788**
3) **Barua-pepe: kengen@tip-offs.com**
4) **Tovuti: www.tip-offs.com**

**MENEJA MKUU, KITENGO CHA UNUNUZI**

KENYA VISION 2030

REPUBLIC OF KENYA

# WIZARA YA ELIMU

## IDARA YA ELIMU YA MSINGI

**MPANGO WA KUHAKIKISHA USAWA KATIKA ELIMU YA SHULE ZA MSINGI KENYA (KPEELP)**

**MRADI NAMBARI. 176867**

## MAOMBI YA ZABUNI

| | |
|---|---|
| **KICHWA CHA KAZI:** | **MINT: USHAURI WA UHAKIKI HURU WA MATOKEO YA SHULE ZILIZOLENGWA ZINAZOPOKEA MISAADA, CHAKULA, UFADHILI WA MASOMO, WALIMU KUTUMWA, MTAALA WA UMILISI NA UTENDAJI NA TATHMINI MSINGI, UJENZI WA MADARASA NA UENDESHAJI WA VYUO VYA MAFUNZO YA WALIMU CHINI YA MPANGO WA KUHAKIKISHA USAWA KATIKA ELIMU YA SHULE YA MSINGI KENYA (KPEELP- P176867)** |
| **MAREJELEO.:** | **MOE/KPEELP/NCB/01/2022-2023** |
| **NJIA YA UNUNUZI:** | **MBINU YA UTEUZI WA GHARAMA NAFUU (LCS)** |

1. Serikali ya Kenya imepokea ufadhili kutoka kwa Benki ya Dunia kugharamia Mpango wa kuhakikisha Usawa katika Elimu ya Shule za Kenya (KPEELP) na inakusudia kutumia sehemu ya mapato ya huduma za ushauri. Programu ina maeneo matatu ya matokeo;
   - **(i) Kusawazisha fursa za kujifunza: Kuboresha matokeo ya kujifunza katika kaunti lengwa,**
   - **(ii) Kuboresha ushiriki wa wasichana katika masomo, na**
   - **(iii) Kuimarisha uwezo wa kutekeleza mageuzi yaliyoanzishwa. Ulipaji Mahususi Umeunganishwa Viashiria (DLIs) vimetengenezwa ili kufuatilia matokeo kwa kila moja ya matokeo matatu maeneo.**
2. Lengo la msingi la mshauri litakuwa ni kufanya uthibitishaji huru kwa uwazi na bila upendeleo wa DLIs kulingana na viambatisho 1 na 2 katika Masharti ya utetezi kama yalivyoainishwa katika itifaki ya awali ya uthibitishaji katika Hati ya Tathmini ya Mradi (PAD). Itatekelezwa bila ushawishi wa Wakala wa Utekelezaji
   Kazi hii inahitaji kampuni ya Ushauri au ubia au Muungano wa makampuni ili kufanya mgawo kulingana na upeo wa kazi angalau mara moja kwa mwaka au kama itakavyohitajika katika kipindi cha miaka minne kuanzia 2023 hadi 2026. Maelezo ya mgawo huo yanapatikana katika Sheria na Masharti (ToR) yaliyopakiwa katika tovuti ya Wizara; **www.elimu.go.ke.**

3. Wizara ya Elimu sasa inakaribisha makampuni ya ushauri yanayostahiki ("Washauri") kuonyesha nia ya kutoa Huduma. Washauri Wanaovutiwa wanapaswa kutoa habari inayoonyesha kuwa wana sifa zinazohitajika na uzoefu unaofaa kutekeleza Huduma. Wataalamu Muhimu hawatatathminiwa katika hatua ya kuorodheshwa.
   Vigezo vya kuorodhesha vitakuwa:
   a) Wakala/kampuni iliyosajiliwa inayotii Ushuru au mshirika na kampuni ya ndani inayofanya kazi chini ya kanuni za Serikali ya Kenya.
   b) Kiwango cha chini cha uzoefu wa miaka mitano katika kufanya kazi zinazofanana au kufanya uchunguzi wa elimu wa ngazi ya kitaifa. Hii inajumuisha uzoefu wa kitaalamu katika kuchanganua data, kuweka kumbukumbu matokeo, na kuunda na kuwasilisha ripoti.
   c) Ushahidi wa ufanisi wa utekelezaji wa kazi zinazofanana ama peke yake au kushirikiana na mashirika husika ya kitaifa au kimataifa i.e Mikataba na mapendekezo kutoka kwa wateja wa zamani.
   d) Ushahidi wa kuwepo kwa ujuzi mchanganyiko unaofaa kutekeleza zoezi la uhakiki unaojumuisha; Wataalamu wa elimu, wataalam wa Maendeleo ya Jamii, Wachumi, Mtakwimu, M&E, Wataalamu wa ICT, Mipango n.k.

4. Tahadhari ya Washauri wanaovutiwa imetolewa kwenye Sehemu ya III, aya,3.14, 3.16, na 3.17 ya Kanuni za Ununuzi za Benki ya Dunia za "Kanuni za Ununuzi kwa Wakopaji wa IPF" zilizorekebishwa Novemba 2020, toleo la 4, zinazoweka bayana sera ya Benki ya Dunia kuhusu migogoro ya hamu.

5. Kampuni ya Ushauri itachaguliwa kwa mujibu wa ***Mbinu ya Uteuzi wa Gharama Nafuu (LCS)*** kwa mujibu wa Kanuni za Ununuzi.

Mashirika Yanayovutiwa yanapaswa kuwasilisha Maonyesho yao ya maslahi ambayo ni lazima yawasilishwe kwa njia ya maandishi yakiambatana na wasifu wa kampuni na nakala za hati husika na uhuda/mapendekezo katika bahasha iliyofungwa wazi iliyo na alama ya kumbukumbu ya nambari ya marejeleo ya mkataba Rejea Na. **MOE/KPEELP/NCB/01 /2022-2023** na kushughulikiwa (ana kwa ana, au kwa barua, au kwa faksi, au kwa barua pepe) kwa;

**Katibu wa Wizara,**
**Wizara ya Elimu, Idara ya Elimu ya Msingi,**
**Attn: Mkuu, Huduma za Usimamizi wa Usambazaji**
**Anwani ya Posta: P.O. Box 30040-00100, Nairobi, Kenya**
**Namba ya posta: +254 Simu: (0)20 318581 Ext.30413 Faksi: 254-020-318581**
**Barua pepe: ppo@education.go.ke**

na kuwekwa kwenye sanduku la zabuni lililo katika eneo la mapokezi la **Jogoo House 'B' Harambee Avenue, mnamo au kabla ya tarehe 7 Februari, 2023** saa **10.00 asubuhi kwa Saa za Kenya.**

Taarifa zaidi zinaweza kupatikana kwa anwani iliyo hapa chini wakati wa saa za kazi kati ya saa 0900 hadi 1700.

**MKUU WA HUDUMA ZA USAMBAZAJI**
**KWA: KATIBU WA WIZARA**

KENYA VISION 2030

# Mfumo wa majitaka mjini Narok wa Sh1.7 bilioni tayari kufunguliwa

NA ANN SALATON (KNA)

Mfumo wa maji taka wa mji wa Narok ambao ulijengwa na serikali kwa gharama ya Sh 1.7 bilioni umekamilika na uko tayari kufunguliwa. Afisa Mkuu Mtendaji wa Shirika la Maji la Kati ya Rift Valley Mhandisi Samuel Oruma anasema kwamba mradi huo uko na uwezo wa kuhudumia takribani watu 200,000 na tayari nyumba 500 zimeunganishwa katika awamu ya kwanza ya kuwezesha shughuli za kiwanda hicho. Ujenzi wa mradi huo, alisema, ulianza mwaka wa 2019 na kukamilika Desemba 2020, huku akiongeza kuwa ulikuwa mradi wa kwanza wa aina yake kukamilishwa ndani ya muda uliowekwa miongoni mwa miradi 22 inayotekelezwa na Mashirika ya Maji katika kaunti hiyo. Mradi huo unaofadhiliwa na Serikali ya Kenya (GoK) kwa ushirikiano na Benki ya Maendeleo Afrika utasimamiwa na kampuni ya Maji ya Narok (NARWASCO). Mhandisi Oruma alithibitisha kwamba kiwanda hicho kiko katika ekari 80 za ardhi zilizonunuliwa na serikali ya kaunti katika eneo la Limanet viungani mwa mji wa. Narok. Afisa Mkuu Mtendaji huyo aliyekuwa akizungumza na wanahabari katika kiwanda hicho cha majitaka alisema kilikuwa cha Kwanza cha aina yake Narok, kikiwa na uwezo wa kutibu lita 3.5 milioni za majitaka kila siku. Kuhusu utunzaji wa mazingira, Mhandisi Oruma alisema kwamba wanashirikiana kwa karibu na Mamlaka ya Taifa ya Kusimamia Mazingira (NEMA) ili kuhakikisha maji yanayoingia katika mto Narok ni salama kwa matumizi ya binadamu. Mpango huo ni afueni kubwa kwa wafanyabiashara na wakazi wa Narok ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakitumia malori ya kuondoa maji taka na kupata hasara kubwa. "Tunatarajia Rais William Ruto kufungua Mradi huu wakati wowote. Tunafurahi kwamba mradi huu umefaulu," alisema Afisa Mkuu Mtendaji huyo.



Picha kutoka juu ya mfumo wa kuzoa maji taka mjini Narok

Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyabiashara Narok David Mpatiany alisema kwamba utekelezaji wa mradi huo unaonyesha wazi jinsi viwango viwili vya serikali vinashirikiana kwa karibu kwa manufaa ya raia. Mradi huo ulijengwa na kampuni ya Sinohydro Corporation Limited kutoka China.

> "Tunatarajia Rais Ruto kuzindua mradi huu wakati wowote. Tuna furahi mradi huu ulifaulu" –Mha Oruma

Serikali ya kaunti itatarajiwa kuutengeneza kila wakati mfumo huo ili kuhakikisha unafanya kazi kuhudumia wakazi kwa muda mrefu.

Mnamo 2017, Rais Mstaafu Uhuru Kenyatta alizindua mradi mkubwa wa maji katika mji wa Narok ambao ulifadhiliwa na serikali ya kitaifa kwa ushirikiano na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Japan kwa gharama ya Sh1.5 bilioni.

REPUBLIC OF KENYA

REREC
RURAL ELECTRIFICATION & RENEWABLE ENERGY CORPORATION

## MWALIKO WA ZABUNI

1. **SHIRIKA LA UNUNUZI**: Shirika la Kuweka Umeme Mashambani na Kusimamia Kawi Asilia, P.O Box 34585 - 00100 Nairobi.

2. **JINA NA MAELEZO YA MKATABA** kama ifuatavyo;

| Namba. | Maelezo ya Zabuni | Dhamana | Kufunga/Kufungua |
|---|---|---|---|
| 1000000899 | Utengenezaji, Uchoraji na Uwekaji Chapa, Uwekaji Machapisho ya Ishara za Mwelekeo kwenye Miradi ya REREC, Uwekaji Chapa ya Kituo cha Nishati na Kutunga na Kuweka Hati za Huduma | 320,000.00 | 27/01/2023 at 10.00am |
| 1000000900 | Utoaji wa Huduma wa Ushauri kwa Mahusiano ya Umma na Shirika la Mawasiliano | 200,000.00 | 27/01/2023 at 10.00am |

3. Zabuni itafanywa chini ya njia ya Kitaifa ya ushindani wazi kwa kutumia zabuni sanifu hati. Zabuni iko wazi kwa Wazabuni wote waliohitimu na wanaopenda.
4. Wazabuni wenye nia waliohitimu wanaweza kupata taarifa zaidi kutoka ofisini saa 8.00 asubuhi-12.45 mchana; kutoka1.45 mchana-4.00 alasiri Jumatatu hadi Ijumaa kwa anwani iliyotolewa hapa chini.
5. Seti kamili ya hati za zabuni inaweza kutazamwa na kupakuliwa na wazabuni wanaovutiwa bila malipo kielektroniki kutoka kwa Tovuti www.rerec.co.ke chini ya hati za zabuni au kupitia tovuti ya ununuzi wa kielektroniki kwa kutumia https://suppliers.rea.co.ke:44300/irj/portal
6. Wazabuni ambao bado hawajasajiliwa na REREC lazima wasajili kampuni zao ili kushiriki katika zabuni kwa kutumia kiungo kilicho hapa chini ambacho kinaweza kupatikana kutoka kwa tovuti **www.rerec.co.ke** Usajili wa Ununuzi-Wasambazaji: ***https://suppliers.rea.co.ke:44200/supportal(bD1lbiZjPTUwMCZkPW1p-bg==)/ bspwdapplication.do#VIEW_ANCHOR-ROS_TOP***
7. Zabuni zote lazima ziambatane na Usalama wa zabuni ulioainishwa kwenye waraka wa zabuni. Mzabuni ataratibu kurasa zote za hati ya zabuni iliyowasilishwa kwa kufuatana. Zabuni zilizokamilishwa lazima ziwasilishwe kwa anwani iliyo hapa chini mnamo au kabla ya tarehe **zilizoonyeshwa hapo juu saa 10.00 asubuhi.**
8. Zabuni za Kielektroniki pekee ndizo zitaruhusiwa. Zabuni zilizochelewa hazitawasilishwa. Zabuni zitafunguliwa mara tu baada ya tarehe ya mwisho na wakati ulioainishwa hapo juu au tarehe ya mwisho na wakati ulioainishwa baadaye. Zabuni zitafunguliwa hadharani mbele ya Wazabuni walioteuliwa wawakilishi wanaochagua kuhudhuria katika anwani iliyo hapa chini na matokeo kutumwa kwa njia ya kielekt.
9. Anwani zilizorejelewa hapo juu ni:

**Anwani kwa ajili ya kupata taarifa zaidi kuhusu hati za zabuni**: kwa ajili ya usalama wa zabuni ya Courier Uwasilishaji kwa ofisi au Sanduku la Zabuni (Kawi Complex, Orofa ya chini). Meneja wa Mawasiliano, Usimamizi wa Mfumo wa Usambazaji, nambari ya simu: 0709193000 na anwani ya barua pepe: **tenders@rerec.co.ke**
**Anwani ya Uwasilishaji wa Zabuni**: Mtandaoni Kupitia **https://suppliers.rea.co.ke:44300/irj/portal**

**Anwani ya Ufunguzi wa Zabuni**. Ununuzi wa kielektroniki wa SAP-SRM

**AFISA MKUU MTENDAJI**
**SHIRIKA LA KUWEKA UMEME MASHAMBANI NA KUSIMAMIA KAWI ASILIA**

KENYA VISION 2030

REPUBLIC OF KENYA

**WIZARA YA KILIMO NA USTAWISHAJI WA KILIMO**

***IDARA YA USTAWISHAJI WA MIMEA***

## MWALIKO KWA WATEULIWA KWENYE BODI YA MAMLAKA YA KILIMO NA CHAKULA (AFA)

**1. UTANGULIZI**

**Kifungu cha 5 (1) (i) cha Sheria ya Mamlaka ya Kilimo na Chakula, Na. 13 ya mwaka 2013 kama ilivyorekebishwa kupitia Sheria ya Bunge (Marekebisho Mseto) ya mwaka 2016** kinaelekeza nafasi ya uanachama wa Bodi ya Mamlaka ya Kilimo na Chakula (AFA) kama inafuata;
***"Watu wanane ambao ni wakulima, wanaowakilisha mashirika ya wakulima katika sekta ndogo za mazao nchini Kenya wateuliwe na Waziri kwa kushauriana na Baraza la Magavana wa Kaunti."***

Kutokana na hilo, Waziri anakaribisha Mashirika ya wakulima yanayofaa ambayo yanawakilisha sekta ndogo za mazao mbalimbali chini ya usimamizi wa Mamlaka hii ambayo ni: **Sukari, Kahawa, Mazao ya Karanga (njugu), Mazao ya Chakula, Mazao ya mboga na maua, Mazao ya Ufumwele, Mazao ya Miraa na Pareto.**

**2. SHIRIKA LA WAKULIMA LINALOTEUWA LAZIMA LITIMIZE VIGEZO VIFUATAVYO:**

a) Shirika hilo lazima liwe na wanachama kutoka katika maeneo yote ya kijiografia ambapo mazao hupandwa Kenya. Shirika linapaswa kutoa orodha ya wanachama wake;
b) Shirika hilo lazima liwe limedumu kwa muda wa angalau miaka 3 katika kipindi cha miaka 3 iliyotangulia;
c) Shirika hilo la wakulima linafaa kutoa katiba au mkataba wake na Kanuni za Muungano na Cheti cha Ushirikishwaji/Usajili na orodha ya maafisa au Wakurugenzi wake;
d) Kila Shirika lazima litoe majina ya watu watatu walioteuliwa ambapo angalau mmoja lazima awe wa jinsia tofauti ili kutimiza sheria ya jinsia ya theluthi moja;
e) Shirika hilo lazima libainishe taaluma ya ukulima ya mkulima aliyeteuliwa k.m. ikiwa ni wa kahawa, mkulima wa mahindi, miwa au mazao mengine;

**3. KUHITIMU KWA WATEULIWA**

a) Wateule lazima watimize sifa za kitaaluma kama ilivyoelezwa chini ya Kifungu cha 5(4)(a) cha Sheria ya AFA, yaani;
   i. **Awe na shahada katika nyanja husika kutoka katika chuo kikuu kinachotambuliwa nchini Kenya;**
   ii. **Awe na tajriba iliyothibitishwa katika usimamizi wa biashara au uzoefu mwingine wa kitaaluma unaofaa;**
   iii. **Awe amehudumu katika nafasi ya usimamizi mkuu kwa kipindi cha angalau miaka sita;**
   iv. **Hapaswi kuwa amehudumu katika shirika moja na mfanyakazi katika miaka mitano iliyotangulia;**
   v. **Akidhi mahitaji ya Sura ya Sita ya Katiba.**
   vi. **Akidhi mahitaji ya mtihani unaohitajika na faafu.**

Majina ya Waliopendekezwa lazima yatumwe kwa Waziri, Wizara ya Kilimo na Ustawi wa Mifugo ili kufika ofisini mnamo au kabla ya **tarehe 24 Januari 2023 Adhuhuri.**

Bahasha za barua lazima ziandikwe kwa hati nzuri ***"NOMINATION FOR AFA BOARD."***

**EAD: KITENGO CHA USIMAMIZI WA USAMBAZAJI/UNUNUZI**
**KWA NIABA YA: WAZIRI**

KENYA VISION 2030






# Serikali kufufua mradi wa mchele uliokwama wa Gamba Tana River

**NA SIMON GURUBA (KNA)**

Serikali imetangaza mipango ya kufufua mradi wa mchele wa Gamba kaunti ya Tana River ambao uliporomoka miaka iliyopita, kuimarisha uzalishaji wa mchele nchini. Kulingana na Katibu wa Idara ya Serikali ya Maeneo Kame (ASAL), Dkt. Idris Dakota, shughuli ya kufufua mradi wa unyunyuzaji wa Tana Delta ambao ulikwama zaidi ya miaka kumi iliyopita imeanza, kwa lengo la kuanza uzalishaji mkubwa wa mchele.

Dkt Dakota alisema kwamba tayari serikali imekarabati mitaro mikuu na midogo katika eneo la Gamba inayopeleka maji katika mashamba ya mchele, na maandalizi yanaendelea katika ekari 100 kuanza uzalishaji wa mchele. Katibu alisema kwamba mradi wa unyunyuzaji wa Tana Delta una uwezo wa hektari 12,000 na mamia ya wakulima katika eneo hilo watapata ajira na manufaa ya kiuchumi mradi huo utakapoanza.

Dakota ambaye alikuwa akikagua mradi huo unavyoendelea alipelekwa Kitere maji yanakotoka , kwenye bwawa na katika shamba ambako maandalizi yanaendelea kwa uzalishaji wa mchele kuanza. Alikuwa ameandamana na Mkurugenzi Mkuu wa TARDA Liban Roba Duba. Aliongeza kuwa watatumia mbinu ya kuhusisha jamii ya eneo hilo katika mradi huo. Dakota alisema kwamba lengo ni kuimarisha matumizi ya mashine katika kilimo na kuunda muundomsingi wa unyunyuzaji ili kuimarisha maisha ya jamii. Watu wa jamii waliohojiwa walishukuru serikali kwa kufufua mradi huo na wakaomba maafisa uharakishwe kwa kuwa utabuni nafasi za ajira na kutatua shida ya uhaba wa chakula katika eneo hilo.

Golo Abdala, mkazi wa kijiji cha of Bandi alisema kwamba mradi huo hautafaidi wakazi wa eneo hilo pekee mbali pia nchi nzima kwa kuwa utaleta pamoja watu wenye ujuzi tofauti kutoka kote.

Alisema kwamba siku zilizopita, mradi huo ulipokuwa ukiendelea, maisha yalikuwa mazuri kwa kuwa watu wengi wangepata mapato na kusomesha watoto wao lakini tangu uliporomoka, maisha yamekuwa magumu.

Osman Korir, mkazi wa kijiji cha Hewani alisema kwamba " Tuko na matumaini sasa baada ya kuona mipango ya kufufua mradi huu kwa kuwa utabuni nafasi za ajira kwa vijana".

---

REPUBLIC OF KENYA

## WIZARA YA KILIMO NA USTAWISHAJI WA MIFUGO

### *IDARA YA USTAWISHAJI WA MIMEA*

### KUAJIRI MWENYEKITI WA BODI YA MAMLAKA YA KILIMO NA CHAKULA (AFA)

| NA. YA MAREJ. YA KAZI: | MOALF/SDCD/02/2022-2023 |
|---|---|

**USULI**

Mamlaka ya Kilimo na Chakula ni Shirika la Umma chini ya Wizara ya Kilimo na Ustawi wa Mifugo lililoanzishwa mahsusi chini ya Kifungu cha 5 cha Sheria ya Mamlaka ya Kilimo na Chakula(AFA), ya mwaka wa 2013. Sheria hiyo ya AFA inaelekeza ujumuishaji wa Sheria kwenye udhibiti na ukuzaji wa Kilimo kwa jumla na kuweka sheria ya majukumu ya Serikali ya Kitaifa na za Kaunti katika Kilimo na masuala yanayohusiana kilimo katika kuendeleza sheria hizo husika za Ibara ya nne ya Katiba.

Kulingana na kifungu cha 5 cha Sheria ya AFA, Wizara ya Kilimo na Ustawi wa Mifugo inatafuta ili kuajiri Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Kilimo na Chakula (AFA)

**WAJIBU NA MAJUKUMU YA MWENYEKITI WA BODI HIYO**

a) Kutoa uongozi wa jumla kwa Bodi;
b) Kutoa uongozi katika kutekeleza Mpango Mkakati na Mkataba wa Utendaji kazi wa Mamlaka hiyo;
c) Kutumia ujuzi wa pamoja wa Bodi na timu ya Usimamizi;
d) Kuunda viungo vinavyofaa kati ya Bodi na timu ya Usimamizi;
e) Kufuatilia na kuongoza katika tathmini ya utendaji kazi wa Mkurugenzi Mkuu;
f) Kutekeleza jukumu muhimu katika kuweka ajenda za vikao vya Bodi na kuendesha vikao hivyo kwa weledi na ufanisi kwa kuongoza hatua ya bodi ya kufanya maamuzi;
g) Kuongoza harakati ya Bodi kujitathmini na kutoa mfano bora wa uongozi kwa wanachama wa Bodi;
h) Kudumisha uhusiano wa karibu lakini huru wa kufanya kazi na Mkurugenzi Mkuu na kuhakikisha usawa unaofaa wa mamlaka kati ya Mkurugenzi Mkuu na Bodi: na
i) Kutekeleza majukumu mengine kama yalivyoainishwa chini ya kanuni za uongozi za Mwongozo kwa mashirika ya serikali na miongozo mingine ya sera za Serikali kwa mashirika ya umma kama inavyotolewa mara kwa mara.

**KUHITIMU NA SIFA MUHIMU**

Mgombeaji anayefaa atahitajika kuwa na sifa zifuatazo za kuhitimu:

1. Awe raia wa Kenya
2. Awe mtu ambaye ana sifa na uzoefu wa taaluma husika katika sekta ya kilimo;
3. Awe na shahada kutoka katika chuo kikuu kinachotambulika nchini Kenya;
4. Awe na ujuzi katika kilimo, fedha, sheria, utawala, usimamizi wa rasilimali watu au utaalamu mwingine wowote kadri mamlaka ya uteuzi itakavyoona unafaa;
5. Awe amehudumu katika nafasi ya uongozi mkuu kwa kipindi kisichopungua miaka sita;
6. Hapaswi kuwa amehudumu katika shirika moja kama mfanyakazi katika miaka mitano iliyopita;
7. Akidhi mahitaji ya Sura ya Sita ya Katiba.
8. Akidhi mahitaji ya mtihani unaohitajika na faafu.

Zaidi ya hayo, ni lazima waombaji watoe Cheti cha Kuidhinishwa na Tume ya Maadili na Kupambana na Ufisadi, Ofisi ya Malipo ya Mikopo, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu na Ulipaji wa Ushuru kutoka kwa Mamlaka ya Ukusanyaji Ushuru ya Kenya pamoja na Cheti cha Maadili Mema.

Maombi yaliyo na Nambari ya marejeleo iliyoandikwa wazi kwenye bahasha na kuambatanisha na Wasifukazi ya kina, Majina ya mawasiliano ya simu ya usiku na mchana na anwani ya barua pepe ya wasimamizi watatu (3), nakala za vyeti vya kiakademia na kitaaluma na ushahidi, yawasilishwe kwa anwani iliyo hapa chini ili kufikia Wizara hii mnamo au kabla ya **tarehe 24 Januari 2023.**

Wawaniaji watakaoorodheshwa pekee ndio tutawasiliana nao. Njama yoyote ya kutaka kupendelewa itasababisha kuchujwa papo kwa hapo.

**NJIA ZETU ZA MAWASILIANO**

**The Cabinet Secretary**
**Ministry of Agriculture and Livestock Development**
**Kilimo House, Cathedral Road**
**P.O.BOX 30028-00100**
**Nairobi,Kenya**
**Simu: +254202718870**
**Barua-pepe: cabinetsecretary@kilimo.go.ke**

KENYA VISION 2030

---

***An ISO 9001:2015 Certified Hospital***

## HOSPITALI YA RUFAA NA MAFUNZO YA MOI

### MASOMO YA USHIRIKA WA MAFUNZO YA BODI YA WATAALAMU WA UPASUAJI (FCS) WA AFRIKA MASHARIKI, YA KATI NA KUSINI (COSECSA)

Hospitali ya Rufaa na Mafunzo ya Moi (MTRH) ni hospitali ya rufaa ya kitaifa yenye huduma mbalimbali, inayohudumia wakaazi wa Magharibi mwa Kenya, maeneo ya Mashariki mwa Uganda, Sudan Kusini, Tanzania na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) na zaidi ya watu milioni 25.

MTRH ni kituo bora cha matibabu ya kitaaluma, mafunzo, utafiti na inashiriki katika upangaji wa afya wa kitaifa kwa kauli mbiu yake, ***"To be a Global Leader in the provision of Exceptional Multi-Specialty Healthcare, Training and Research"***.

Hii ni FCS ya kuishi muda wote kwa miaka mitatu (3) (Upasuaji wa Kawaida, Upasuaji wa Neva/Ubongo, Mifupa, au Upasuaji wa Watoto), chini ya mpango wa mafunzo wa COSECSA. Uthibitisho wa usaidizi kamili wa kifedha kutoka kwa mwajiri wako kwa muda wa kozi hii ni wa lazima. Hakutakuwa na mshahara au fidia kwa nafasi hizi.

Nafasi (8) zinazopatikana ni kama zifuatavyo:

| S/No | Taaluma | Idadi ya Nafasi |
|---|---|---|
| 1 | Upasuaji wa Jumla | 2 |
| 2 | Upasuaji wa Mfumo wa Neva (Neurosurgery) | 2 |
| 3 | Uhazigi (Upasuaji wa Mifupa na Misuli) yaani Orthopedics | 2 |
| 4 | Upasuaji wa Watoto (Pediatrics) | 2 |
| | **Jumla** | **8** |

Sharti wawaniaji waonyeshe uthibitisho wa mahitaji yafuatayo:

1. Cheti cha kukamilisha cha Mwanachama wa College of Surgeon (MCS) Sehemu ya II Mtihani au barua/baruameme kutoka kwa Sekretarieti ya COSECSA inayoonyesha kukamilisha kwako.
2. Shahada ya Udaktari na Shahada ya Upasuaji (M.B.Ch.B) au shahada sawia, kutoka kwa taasisi inayotambuliwa na Baraza la Matabibu na Madaktari wa Meno.
3. Uthibitisho wa Kusajiliwa na, na Kusalia katika rejista ya, Baraza la Matabibu na Madaktari wa Meno la Kenya.
4. Ushahidi wa ufadhili kutoka kwa Mwajiri/Kaunti/Mwenyewe.
5. Barua mbili za mapendekezo, moja kutoka kwa msimamizi wa karibu na nyingine kutoka kwa Msimamizi wa Hospitali k.m. Msimamizi wa Matibabu.
6. Barua ya maombi inayoonyesha maslahi yako ya kazi.
7. Bima halali ya Kitaaluma, na Bima ya Matibabu kwa miaka mitatu (3).
8. Wagombeaji watahitajika kulipa ada ya kutuma maombi isiyorejeshwa ya Ksh.5,000/= kwa nambari ya akaunti ifuatayo, na kuambatanisha risiti ya malipo kwenye maombi hayo:

**Account Name : Moi Teaching & Referral Hospital**
**Account No : 1103464329**
**Bank : Kenya Commercial Bank**
**Bank Branch : Eldoret West**

Kwa maelezo zaidi tembelea tovuti yetu **www.mtrh.go.ke.**

Wagombeaji wanaovutiwa, ambao wanatimiza vigezo hivyo, wanafaa kutuma maombi kwa kutuma wasifukazi ya kina, nakala husika za kiakademia/ kitaaluma na barua ya mapendekezo kutoka kwa wasimamizi watatu (3) wawili (2) wao lazima watoke kwenye taaluma yako.

Tuma maombi kwa baruapepe **ceo@mtrh.go.ke, aruasaw@gmail.com** na **ceosoffice@mtrh.go.ke.**

**CHIEF EXECUTIVE OFFICER**
**MOI TEACHING AND REFERRAL HOSPITAL**
**CHANDARIA CANCER AND CHRONIC DISEASES CENTRE**
**P.O BOX 3-30100**
**ELDORET**

Siku ya mwisho ya kuwasilisha maombi ni Ijumaa, tarehe 24 Februari, 2023 saa kumi na moja kamili jioni. Wagombeaji walioorodheshwa pekee ndio wataalikwa kwenye usaili.

**AFISA MKUU MTENDAJI**
**HOSPITALI YA RUFAA NA MAFUNZO YA MOI**

KENYA VISION 2030

COVID-19
“ Virusi havitembei, watu huvisambaza, tukiacha kutembea, virusi vitakufa”
HOMA
KIKOHOZI
KUSHINDWA KUPUMUA
MAUMIVU KOONI
KUUMWA NA KICHWA

# Serikali kuharakisha ujenzi wa bwawa kubwa la Thwake

NA PATRICK NYAKUNDI NA RONALD RONO (KNA)



Waziri wa Maji Alice Wahome (kati) akiandamana na gavana wa Makueni, Mutula Kilonzo Jnr (wa pili kulia) na katibu maji Dkt Paul Ronoh (kulia) wakati wa ukaguzi wa mradi wa ujenzi wa bwawa la Thwake Dam



Serikali ya Kitaifa itaharakisha ukamilishaji wa sehemu iliyobaki muhimu ya mradi wa Bwawa la Thwake ambalo awamu yake ya kwanza inaendelea kujengwa ili kuhakikisha utoshelevu wa chakula katika eneo hilo Kusini Mashariki. Waziri wa Maji, Usafi na Unyunyuzaji Bi Alice Wahome alifichua kwamba wizara yake imeunda timu ya utekelezaji kufuatilia na kuharakisha ujenzi wa bwawa hilo ili kuhakikisha unakamilika chini ya awamu ya kwanza kufikia Juni, 2024.

“Tuko na timu ya utekelezaji katika makao makuu ya Wizara na itakuwa ikiripoti kwangu na Katibu Dkt . Paul Ronoh kila baada ya miezi mitatu kuhusu bwawa linavyoendelea,” alisema.

“Tunafuata muda uliowekwa na hatutakubali uzembe wowote au ucheleweshaji,” aliongeza Wahome katika ziara ya kukagua bwawa hilo.

“ Ninatumaini mwanakandarasi atatia bidii kutimiza muda uliowekwa. Lazima tulinde mabilioni ya pesa za mlipa ushuru ambazo zimetumiwa katika mradi huu, hatutakubali visingizio vyovyote,” alionya Waziri.

Kuhusu utoshelevu wa chakula, Wahome alisema kwamba kaunti tatu za Ukambani za Kitui, Machakos na Makueni zimejaliwa michanga yenye rotuba na serikali imejitolea kutoa maji ya kutosha ya kunyunyiza mashamba kuinua uzalishaji wa chakula katika eneo hilo.

Alifichua kuwa Rais William Ruto anasubiri kufungua bwawa hilo linalotarajiwa kunufaisha wakazi zaidi ya 1.2 milioni katika eneo la Kusini Mashiriki.

Kuhusu uchafuzi, Wahome alisema kwamba tume mpya iliyoundwa ya Mito ya Nairobi itashirikiana na mashirika yote yanayohusika na Wizara kusafisha mto Athi na kuadhibu wanaouchafua.

“Mojawapo ya majukumu ya wizara yangu ni kuhakikisha kwamba Wakenya wanapata maji safi na salama. Viwanda vinavyotoa kemikali na shughuli za kilimo kwenye kingo za mto lazima zikomeshwe mara moja,” alisema huku akihimiza vyombo vya habari kuongoza katika kampeni hiyo kwa kufichua wanaohusika. Wahome alihimiza mwanakandarasi kuzingatia haki za binadamu akifanya ulipuaji na kuhakikisha jamii inanufaika na nafasi za kazi za mikono na za ujuzi zilizopo.

Waziri alifichua kwamba kazi ya kuweka dawa maji itafanywa wakati bwawa litakuwa likijazwa maji na akaongeza kuwa mradi huo ungekuwa umeharakishwa lakini mchakato wa kutafuta Sh37 bilioni za kazi ya ujenzi, kupatia makao watu walioathiriwa na mradi huo (PAPs), masuala ya kisheria na changamoto zingine za ujenzi zilifanya uendeshwe pole pole. Akizungumza wakati wa ziara hiyo Gavana wa Makueni Mutula Kilonzo Jnr alihimiza wizara kukarabati barabara za kuingia eneo hilo.

> “ Mojawapo ya majukumu ya wizara yangu ni kuhakikisha Wakenya wanapata maji safi kila mahali,” -Waziri Wahome

# Matumaini ya utoaji huduma bora za serikali mfumo mpya wa kusimamia wafanya kazi ukizinduliwa

NA JOSEPH NG'ANG'A (KNA)

IDARA ya Serikali ya Utumishi wa Umma imezindua mfumo wa Habari za Wafanya kazi wa Serikali (GHRIS) muundomsingi ulioboreshwa na mfumo wa pamoja wa wafanyakazi (UHR) unaolenga kutoa huduma bora katika viwango viwili vya serikali.

Waziri wa Utumishi wa Umma na Jinsia Aisha Jumwa alisema kwamba kuanzishwa kwa muundomsingi wa ICT kumejiri wakati unaofaa ambao serikali inakumbatia dijitali kupitia ubunifu na kujenga uwezo kupitia mfumo mkubwa wa dijitali.

Akizungumza katika Taasisi ya Mafunzo ya Serikali wakati wa kuzinduliwa kwa mfumo huo, Jumwa alisema katika maadhimisho ya 59 ya Jamhuri Dei 2022, Rais William Ruto katika hotuba yake alisema hali ya baadaye ya nchi itajikita katika tekinolojia na ubunifu.

“Mfumo mkubwa wa dijitali utatekeleza jukumu muhimu katika kuwezesha ufanisi mkubwa wa nguzo nne za afya, kilimo, biashara ndogo na za kati ba fedha, sawa na kuinua ukusanyaji wa mapato kupitia kuboresha mifumo ya VAT,” alisema. Waziri alisema kwamba lengo kuu la kuanzisha UHR na kuboresha GHRIS ni kutimiza wito wa rais wa kufanya huduma za

**Aisha Jumwa**

serikali kuwa za dijitali.

“Kama sehemu ya kufanya huduma za serikali kuwa za dijitali, wizara yangu pia inaboresha muundomsingi wa ICT ili kuinua utoaji wa huduma chini ya mpango wa Huduma Kenya,” Jumwa alisema.Kama kivumishi cha kuafikia ajenda yake ya kiuchumi na maendeleo ya jamii na kutekeleza manifesto ya Kenya Kwanza, serikali inahitaji huduma ya umma inayofahamu IT, kwa kukusanya data bila kuchelewa na uwezo wa kufanya maamuzi haraka, alieleza.

“Kuanzishwa kwa mifumo hii mipya kunaashiria mwanzo wa safari ya kubadilisha usimamizi wa habari za wafanyakazi katika utumishi wa umma kwa kuimarisha upatikanaji wa habari katika njia zinazotakiwa na kuhakikisha utimizaji na usimamizi bora wa wafanyakazi,” alisema Waziri. Aliagiza kwamba mashirika ya umma ambayo mishahara inalipwa moja kwa moja kutoka Hazina Kuu au moja kwa moja kutoka pesa zinazotengwa na serikali yahamishie mifumo yake ya wafanyakazi na mishahara hadi mifumo hiyo mipya alivyoelekeza Mkuu wa Utumishi wa Umma. Jumwa alisema kwamba wizara yake itahakikisha uhamaji wa mashirika ya serikali hautatizika ndani ya muda uliowekwa wa hadi Julai 1, 2023. Katibu wa Idara ya Serikali ya Utumishi wa Umma Amos Gathecha alisema kwamba waligundua kuwa taasisi za umma zinatumia mifumo tofauti na huru ya habari za wafanya kazi ambayo usimamizi wake ni dhaifu.

PCF
POLICYHOLDERS COMPENSATION FUND
Dhamana ya Bima Yako

## NAFAZI NZURI ZA KAZI

Policyholder Compensation Fund (PCF) ni Shirika la Umma linaloendeshwa kwa kuzingatia sehemu ya 179 ya Sheria za Bima (Cap 487) na Kanuni za Bima (Policyholder Compensation Fund) (Marekebisho) za mwaka wa 2014. Hazina hii ilianzishwa kwa lengo kuu la kutoa fidia kwa walalamishi wa mtoaji bima ambaye yuko chini ya Usimamizi wa Kisheria na lengo lingine ni kuongeza imani ya umma kwa jumla kwenye sekta ya bima.

Hazina hii inaendesha Mpango wa Vijana Wataalamu (YPP) wa mwaka mmoja (1) ili wanaoshiriki kujizoesha na nyanja zao mbalimbali za kitaaluma na kuimarisha uwezo wa Hazina hii kutekeleza majukumu yake. Kwa mwaka wa 2023, Hazina hii inatafuta ili kuajiri watu waliohitimu na wenye ujuzi ili kujaza nafasi hizi mbili (2) zilizo wazi katika mpango huo.

| Marej. ya Kazi | Jukumu/Cheo | Fani ya Kitaalamu | Idadi ya Nafasi |
|---|---|---|---|
| PCF/01/2023 | Mtaalamu Mchanga | Mawasiliano ya Shirika | 1 |
| PCF/02/2023 | Mtaalamu Mchanga | Fedha & Uhasibu/ Ukaguzi | 1 |

**Kanuni za Kazi**

Mkataba wa mwaka mmoja (1) unaorudiwa tena mara moja kutegemea utendakazi na uwepo wa Fedha.

**Utamaji Maombi**

1. Maelezo ya kina ya kazi, mtu anayehitajika na jinsi ya kutuma maombi yanapatikana kwenye tovuti www.pcf.go.ke/careers
2. Sharti maombi yote yapokelewe mnamo au kabla ya tarehe 23 Januari 2023 kufikia saa kumi na moja kamili jioni.
3. PCF ni mwajiri wa fursa sawa. Njama yoyote ya kutaka kupendelewa itasababisha kuchujwa papo kwa hapo. Wanawake, Vijana na Walemavu wanahimizwa kutuma maombi.
4. Maombi ya kazi za PCF hayalipishwi ada yoyote
5. Wagombeaji walioorodheshwa pekee ndio tutawasiliana nao.

KENYA VISION 2030






# Daktari Mkenya ashinda wawaniaji 2000 na kutwaa tuzo la uongozi

**NA JUDY SHERI (PCO)**

Daktari wa matibabu wa Kenya ametuzwa kwa mchango wake kwa mipango ya Huduma ya afya nchini na kote ulimwenguni.

Dkt Pauline Wairimu, mkuu wa Vifaa vya Matibabu na Utambuzi katika Bodi ya Kuthibiti Dawa na Sumu, alishindwa Tuzo la Uongozi Bora wa Afya Health 2.0 miongoni mwa madaktari 2000 waliotuma maombi katika kongamano la Afya 2.0 lililofanyika Desemba 2022 Las Vegas, Amerika. Kongamano la Afya

2.0 ni jukwaa la kipekee la aina yake linaloleta pamoja wataalamu wa afya wenye ari na huangazia maendeleo ya hivi punde na ubunifu katika sekta ya afya kote ulimwenguni. Shabaha ya kongamano hilo ni kuinua ubadilishanaji wa ufahamu miongoni mwa wakuu wa afya wenye maono ambao huwa wanatafuta suluhu kwa changamoto kuu za utoaji wa huduma za afya. Hafla hiyo ya kimataifa huwa inaleta pamoja wataalamu wakuu kutoka sekta za kibinafsi na umma za afya. Dkt Wairimu kutoka Kenya alituzwa pamoja na wengine wenye maono na mashirika yanayoongoza ambayo yamekuwa na athari chanya kwa huduma za afya kote ulimwenguni kupitia michango yao

**2022**
**Mwaka kongamano la Health 2.0 liliandaliwa**

muhimu. Wataalamu waliotuzwa walitekeleza jukumu muhimu katika kupunguza gharama ya matibabu, kuimarisha ufikiaji na ubora wa afya, huku wakitambua bidhaa na huduma ambazo zimeinua utendaji katika mifumo ya huduma za afya katika maeneo yao.

Kwa muktadha huu, jukumu la Dkt Wairimu kitaifa katika PPB na mchango wake kwa Bara la Afrika kama mwenyekiti wa African Medical Devices Forum (AMDF), chini ya usimamizi wa Mpango wa Uwianishi wa Uthibiti wa Dawa Afrika (AMRH), ndani ya Muungano wa Afrika, na pia akiwa aliwakilisha Kenya katika Kongamano la Afya Ulimwenguni, Shirika la kuu zaidi la kufanya maamuzi ya afya, Geneva, kulimfanya kufana.

---

KNTC
Kenya National Trading Corporation Ltd.

## TENDER ADVERTISEMENT

Kenya National Trading Corporation (KNTC) is a State Corporation in the Ministry of Trade Investments and Industry with a mandate to provide Procurement agency services to the Government, promote wholesale and retail trade through distribution of essential commodities within the country with flagship products including Fertilizers, Rice, Assorted Farm implements, Assorted Hardware among other general supplies. KNTC also provides Warehousing space and services to the general public besides supporting local SME's through finding local and export markets for their products.

The Corporation invites sealed tenders from eligible bidders for provision of Information System Audit.

| No. | Tender No. | Tender Description | Eligibility |
|---|---|---|---|
| 1. | TENDER/KNTC/017/2022-2023 | Tender for provision of Information System Audit. | Open |

Bidders are requested to view and download more details on the tender documents from the Corporation's website **www.kntc.co.ke**.

Completed Tender documents must be submitted in a plain sealed envelope clearly marked Eg-**'TENDER NO:** deposited in the Tender Box at KNTC Head Office, Ground floor, Yarrow Road Complex, Off Nanyuki Road, Industrial Area, Nairobi on or before **24th January, 2023** at **10:00 am,** addressed to:

**The Managing Director**
**Kenya National Trading Corporation**
**P.O. Box 30587-00100**
**NAIROBI**

**NB: Hard copies can be purchased at Ksh at 1000.00 from our head office during working hours from 8.00am – 5.00pm.**

**Late Bids will NOT be accepted**

---

REPUBLIC OF KENYA

# WZARA YA MASUALA YA VIJANA, SPOTI, NA SANAA

***IDARA YA MASUALA YA VIJANA***

## OMBI LA KUONYESHA NIA (UTEUZI WA WASHAURI BINAFSI)

| | |
|---|---|
| **NCHI** | **KENYA** |
| **Jina la Mradi** | **Kenya Youth Employment and Opportunities Project** |
| **Na. ya Mkopo/Credit No./ Grant No.** | **5812-KE** |
| **Jina la Kazi** | **Mtaalamu wa Ufuatiliaji na Tathmini** |
| **Na. ya Marejeleo** | **KE-MPYG-324737-CS-INDV** |

**USULI**

Serikali ya Kenya imepokea ufadhili kutoka kwa Benki ya Dunia ili kugharamia Mradi wa Kazi na Fursa kwa Vijana wa Kenya (KYEOP) na inakusudia kutumia baadhi ya fedha hizo kwa ununuzi wa Huduma za Ushauri (Mtaalamu wa Ufuatiliaji na Tathmini). Washauri binafsi wanaovutiwa wanaelekezwa kwenye aya ya 1.9 ya Miongozo ya Benki ya Dunia: Uteuzi na Kuajiriwa kwa washauri binafsi [chini ya Mikopo ya IBRD na Madeni & Ruzuku ya IDA] ya Wakopaji wa Benki ya Dunia ya Januari, 2011 na iliyorekebishwa Julai, 2014 na kubuni sera ya Benki ya Dunia kuhusu migongano ya maslahi.

Serikali ya Kenya (GoK), kupitia kwa Wizara ya Maswala ya Vijana, Michezo, na Sanaa inatafuta huduma za Mtaalamu wa Ufuatiliaji na Tathmini (Mshauri) ili; Kubuni mpango madhubuti wa uwasilishaji wa Ripoti ya Kukamilika kwa Utekelezaji (ICR) wenye utaratibu na watu wanaowajibika kwa utoaji wa data kutoka kwa kila Mashirika ya Utekelezaji wa mradi (IAs), Kutayarisha ICR ya Mradi kulingana na muundo uliowekwa. Ripoti hiyo inapaswa kujumuisha takwimu zote za mradi zilizokusanywa na Mashirika ya Utekelezaji wa Miradi (IAs) ukiwemo Mfumo wa Taarifa za Usimamizi (MIS), Kufuatilia uajiri wa wanaonufaika na mradi, Kusimamia Utafiti wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Hazina ya Government Catalytic Fund na majukumu mengine yoyote kama yatakavyoelekezwa na Mratibu wa Mradi wa Kitaifa (NPC). Mshauri huyo atakuwa na makao yake Nairobi, Kenya, lakini atasafiri hadi katika kaunti zingine.

Mshauri atateuliwa kwa kufuata mbinu ya Uteuzi wa Washauri Binafsi iliyobainishwa katika Miongozo ya Benki ya Dunia inayotumika: Uteuzi na Kuajiriwa kwa Washauri. Hadidu ya Rejea ya Kina (ToR) kwa ushauri huo inaweza kupakuliwa kutoka kwenye https://kyeop.go.ke/tenders/

Wagombeaji wanaovutiwa na ambao wanastahiki wanaweza kupata maelezo zaidi kutoka kwa Ofisi ya Usimamizi wa Usambazaji ya Mradi huu, Orofa ya 3 Chumba Na. 321 katika ofisi za KYEOP, Bruce House, Standard Street, wakati wa saa rasmi za kazi (saa mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na moja kamili jioni). Nakala za REOI zilizojazwa kikamilifu (kuorodhesha na kupigwa mhuri/kusaini kila ukurasa) na zilizowekwa katika bahasha safi iliyofumwa na kuandikwa wazi nambari ya marejeleo ya zabuni zinafaa kuelekezwa kwa Principal Secretary, State Department of Youth Affairs P. O. Box 30050 – 00100, Nairobi, Kenya na kutumbukizwa kwenye Sanduku la zabuni katika Ghorofa ya 3 ya Bruce House ili kupokelewa mnamo au kabla ya **Jumanne tarehe 24 Januari 2023, saa nne kamili asubuhi.**

REOI hayo yatafunguliwa mara tu baada ya hapo mbele ya wagombeaji au wawakilishi wao katika Ukumbi wa mikutano wa KYEOP, Bruce House, 3rd Floor Standard Street Nairobi.

**KATIBU WA WIZARA**
**IDARA YA MASUALA YA VIJANA**

KENYA VISION 2030

---

KAA Kenya Airports Authority

## NOTISI YA KUTANGAZA TENDA

Kenya Airports Authority inaalika maombi ya tenda kutoka kwa taasisi kwa tenda zifuatazo: -

| NAMBARI YA MAREJELEO | MAELEZOYA TENDA | MKUTANO ZIARA YA ENEO/ KWA HIARI | TAREHE YA KUFUNGA/ KUFUNGUA |
|---|---|---|---|
| KAA/OT/MLD/0081/2022-2023 | Shughuli za ukarabati kuzuia maji ya mvua kuingia uwanja wa ndege wa Malindi | Wanaotuma maombi wahitajika kuwasiliana nasi kupitia tenders@kaa.go.ke kabla ya kutembelea maeneo ili kuhakikisha mahitaji ya kutotangamana yanazingatiwa. | 24/1/2023 saa 5.00 asubuhi. |
| KAA/OT/JKIA/0090/2022-2023 | Kununua na kupeleka vipuri vya mitambo ya ukaguzi ya T1E na T2 katika Jomo Kenyatta International Airport" | N/A | 25/1/2023 saa 5.00 asubuhi. |
| KAA/OT/SEC/0086/2022-2023 | Utoaji wa Huduma za Usalama na Ulinzi katika Kenya Airports Authority<br>• ***Lot 1: Jomo Kenyatta International Airport, Embakasi Staff Houses na KAA Headquarters***<br>• ***Lot 2 Northern Region (Isiolo,Nyaribo and Nanyuki)***<br>• ***Lot 3 North Rift Region (Eldoret Int Airport, Eldoret Airstrip, Lodwar Airstrip)***<br>• ***Lot 4 Western Region (Kakamega, Migori, Suneka & Kabunde Airstrips)*** | N/A | 26/1/2023 saa 5.00 asubuhi. |

Maelezo kuhusu notisi hizi za tenda na stakabadhi za kuelezea kwa kina mahitaji, taratibu za kujaza tenda zinapasa kuchukuliwa kutoka kwa tovuti yetu https://www.kaa.go.ke/corporate/procurement/ au https://suppliers.kaa.go.ke/irj/portal au Public or Procurement Information Portal katika www.tenders.go.ke ***bila malipo***

Wanaotuma maombi wanashauriwa kuwa maombi yote yanafanywa mtandaoni kupitia kwa wavuti https://suppliers.kaa.go.ke/irj/portal. Kwa habari au maelezo zaidi, tafadhari wasiliana nasi kupitia, tenders@kaa.go.ke

Kufanya kampeni ya kupata tenda binafsi au kupitia maajenti kutafanya ombi lako litupwe nje.

**MKURUGENZI MKUU/CEO**

KENYA VISION 2030

JANUARI 10, 2023

# MyGov.

NAIROBI-KENYA I TOLEO No. 26/2022-2023

A PUBLICATION OF
**Government Advertising Agency**
Telposta Towers, Kenyatta Ave/ Koinange Street
P.O Box 30025-00100,
Nairobi Kenya
Telephone: (+254) 4920000 / 1
E-Mail: info@information.go.ke

## Vikundi vya wanawake katika Laikipia vyanufaika na uuzaji wa Aloe Vera nje

**NA MUTURI MWANGI (KNA)**

Vikundi vya wanawake katika kaunti ndogo ya Laikipia Kaskazini vitanufaika kupitia kilimo cha Aloe Vera kufuatia kupitishwa kwa Sheria ya Bunge kuruhusu wanawake kumiliki ardhi yao.

Huku umiliki wa ardhi ukiwa changamoto hasa kwa wanawake kutoka jamii za wafugaji, kupitishwa kwa sheria ya Ardhi ya Jamii 2016, kumefanya wanawake wengi kusajiliwa kama wamiliki wa ardhi.

"Awali, walikuwa wakisema iwapo mumeo ni mwanachama wa jamii ungekuwa chini yake, jambo ambalo liliathiri wanawake vibaya, hasa wajane. Sasa sisi ni wanachama wa ardhi ya jamii," alisema mkurugenzi wa Ilpolei Twala Cultural Manyatta Women group Rosemary Nenini.

Alifichua kwamba baada ya mpito kutoka mashamba hadi ardhi ya jamii, wanawake wameweza kushiriki shughuli za kuwaletea mapato kama kilimo cha Aloe Vera wanayouza ng'ambo.

"Kupitishwa kwa Sheria ya Ardhi ya Jamii ya 2016 kumetusaidia pakubwa kwa sababu majina ya wanawake wote yako katika sajili za ardhi tofauti na awali. Ninawaambia wanaume, hatupeleki ardhi popote, itabaki kuwa ya jamii na watu wote watanufaika," Nenini alisema.



**Mwanzilishi na mkurugenzi wa Ilpolei Twala Cultural Manyatta Women Group Rosemary Nenini *akiwa katika shamba lao la Aloe Vera eneo la Ilpolei, Laikipia North.***

> Kilo ya Aloe Vera inauzwa kwa kati ya Sh380 na Sh400 Uingereza na matawi mawili ni kilo-Nenini

Alisema kwamba baada ya kupata ardhi ya jamii, wanawake wengi wa Laikipia Kaskazini wamenufaika wakiwemo 203 kutoka kikundi cha wanawake ambao wananufaika moja kwa moja na kilimo cha Aloe Vera Ilpolei.

"Tunapanda Aloe Vera, ambayo ni ya kienyeji kwa sababu inatumiwa kama dawa. Kwa sasa hivi, aloe yetu inaletea wanawake wa Twala pesa nyingi kwa sababu tunauza matawi mabichi kwa kampuni ya Uingereza ya Lush Cosmetics," anafichua.

Aloe Vera ambao ni mumea ulio na maji unajulikana kwa kutumiwa kama dawa na unaweza kutumiwa katika kidonda, kutunza ngozi miongoni mwa manufaa mengine.

Ni shughuli ambayo wakulima wanategemea hasa katika maeneo yenye joto ya Kenya, alisema mkurugenzi huyo.

Nenini alisema kwamba kabla ya kupata soko la kuuza aloe vera yao nje ya nchi mwaka wa 2013, walikuwa wakibadilishana zao hilo na mbuzi za waume zao. Wanaume walikuwa wakitumia mumea huo kutegeneza pombe waliyochanganya na asali maarufu kama "muratina", alieleza. "Awali, mizizi ilikuwa ikitumiwa na wanaume wa Wamaasai kutengeneza pombe ya kitamanduni ikichanganywa na asali. Lakini shirika la Laikipia Permaculture lilitufunza jinsi ya kupanda na kutuunganisha na Lush Cosmetics ya Uingereza," alisema na kuongeza kuwa uuzaji wa Aloe vera ulipungua kwa sababu ya Covid.

Kilo moja ya Aloe Vera inauzwa kwa kati ya Sh380 na Sh400 Uingereza na ni majani mawili tu yanayotosha kilo moja.

## Serikali kuanza kampeni ya kutangaza na kuvumisha maeneo ya kitalii Victoria

**NA DAVIS LANGAT NA NICHOLAS OTIENO**

Serikali imeanza kutenga na kutangaza vivutio vya kitalii katika Ziwa Victoria na visiwa vyake katika juhudi za kubadilisha uchumi wa eneo hilo.

Waziri wa Utalii,Wanyama Pori na Urithi, Peninah Malonza alisema kwamba mengi ya maeneo hayo hayajatangazwa ipasavyo kuweza kuvutia wageni wa kimataifa.

Akizungumza baada ya kuongoza makala ya kumi na moja ya tamasha ya kitamanduni ya Rusinga katika kaunti ya Homa Bay, Malonza alisema kwamba serikali inataka kuhakikisha vivutio vya utalii katika Ziwa Victoria vimetumiwa kikamilifu.



**Waziri Peninah Malonza nguo nyeupe) aweka shada la maua katika kaburi la Tom Mboya.**

Maeneo ya kuvutia watalii katika eneo hilo ni pamoja na Tom Mboya Mausoleum ambako aliyekuwa mpiganiaji uhuru na Waziri wa Leba Tom Mboya alizikwa. Ziwa hilo pia lina uwezo mkubwa wa michezo ya majini na limejaliwa fuo zenye changarawe nyeupe katika visiwa vya Takawiri.

Kisiwa cha Rusinga ambapo binadamu wa zamani , Proconsul africanus alivumbuliwa, ni kituo kingine cha kuvutia. Ziwa lina madhababu katika visiwa vya Mfangano, Rusinga, Ngodhe na Takawiri.

Malonza alisema kwam ba njia bora ya kutumia uwezo wa kutalii katika eneo hilo ni kutangaza maeneo hayo kwa watalii wa humu nchini na wa kigeni.

Waziri alisema alitembelea eneo hilo na kugundua maeneo mengi ya kuvutia watalii ambayo hayajatumiwa vilivyo.

## KWA UFUPI

### Waziri asifu kituo kipya cha mafuta cha Kipevu

Kituo kipya cha mafuta cha Kipevu Oil Terminal (KOT) kilichogharimu Sh40 bilioni kinatarajiwa kuwezesha Kenya kuongeza maradufu uwezo wake wa kupitisha bidhaa za mafuta hadi ukanda wa Mashariki na Kati ya Afrika.

Akizungumza katika ziara ya kituo hicho, Waziri wa Kawi na Petroli Davis Chirchir alitaja kituo hicho kama kitakachobadilisha nchi Kenya inapoelekea kuwa inayoongoza kwa kushughulikia bidhaa za petroli katika ukanda wa Afrika Mashariki na Maziwa Makuu.

"Kenya iko katika nafasi nzuri ya kuongoza kwa bidhaa za petroli katika eneo hili kufuatia uwekezaji mkubwa katika sekta hiyo," alisema Chirchir.

Alisema kwamba serikali inataka kusaidia uwekezaji katika uhifadhi na uondoaji wa kutoshana na uwezo wa kituo hicho kipya.

Aidha, alifanya ziara ya kujifahamisha katika vituo vya Kipevu Oil Terminal 1 na 2 na Shimanzi Oil Terminal.

Waziri alisema kwamba kituo kipya cha mafuta cha Kipevu ni uwekezaji mkubwa wa nchi na hatua zitachukuliwa kuimarisha kituo hicho ili kufanya nchi kuwa kitovu katika eneo hili na zaidi.

Kituo hicho kipya kinapatikana katika Bandari ya Mombasa, mkabala na kile cha zamani cha mafuta cha Kipevu kilichojengwa 1963.

Mradi huo mpya unajumuisha kituo kimoja cha kisiwani kilicho na maeneo manne ya meli ya urefu wa mita 770 na moja la mashua katika upande wa Westmont lenye vifaa vya kutia.

Pia kina mabomba matano ambayo sehemu yake inafika mita 26 chini ya bahari kuruhusu uchimbaji wa eneo hilo siku zijazo bila kuvuruga mabomba hayo. Kuna sehemu zilizotengewa kila aina ya bidhaa za mafuta na mabomba sita kila moja ikiunganisha kituo hicho na kampuni ya kusafisha mafuta ya Kenya Petroleum Refineries Limited na matangi ya kuhifadhi mafuta ya kampuni ya Mabomba ya Kenya.

Kituo hicho kipya kiko na maeneo manne ya kutua meli kuweza kushughulikia bidhaa sita tofauti za uagizwaji na uuzaji nje.

*Na Mohammed Hassan (KNA)*

### Wizara ya Kawi yakomboa hektari 1600 za ardhi nchini

Wizara ya Kawi na Petroli, kupitia Mpango wa Hazina ya Sekta ya Kawi kuwajibikia Jamii Kimazingira (KEEP) imekomboa jumula ya hektari 1,600 za ardhi katika sehemu kadhaa za nchi. Waziri wa wizara hiyo Davis Chirchir alisema kwamba shughuli za pesa za Hazina hiyo zinazohusu upanzi wa miti kulinda mazingira na kuhifadhi maeneo ya maji kwa mabwawa ya kuzalisha stima.

Kupitia hili, Chirchir alisema kwamba, wizara inashirikiana na Huduma ya Misitu Kenya (KFS) na wadau wengine na akaongeza kuwa zaidi ya wanachama 1200 wa jamii wamekuwa wakihusishwa katika mradi huo tangu ulipoanzishwa 2007.

Alisema hayo akiwa eneo la Chebitet katika msitu wa Maasai Mau alipoongoza wakazi wa Narok kupanda miti ipatayo 29, 000 katika hektari 2908 za ardhi ya msitu.

Hafla ya upanzi wa miti ilihudhuriwa na Gavana wa Narok Patrick Ntutu, Katibu wa wizara ya Utalii John Olotua, katibu wa wizara ya kilimo Julius Korir, mbunge wa Narok Kusini Kitilai Ntutu, na mbunge wa Narok Mashariki Ken Aramat na kamishna wa kaunti ya Narok Isaac Masinde miongoni mwa wengine.

Miongoni mwa miradi mikubwa iliyofaulu ni upanzi wa miti katika msitu wa Enoosupukia kaunti ya Narok , ambako wizara yake ilipanda miche 480, 000 kaika hektari 300 ambao ulikuwa mnara wa maji bila msitu, unahudumia visima vya nguvu za mvuke vilivyo chini ya mlima.

"Dunia inakabiliwa na mzozo mara tatu wa mabadiliko ya tabia nchi, ukataji wa miti na uchafuzi. Kupanda miti ni sehemu ya hatua za muda mrefu za kusaidia kukabili mizozo huu," alisema.

Kupitia Hazina ya KEEP, waziri alisema, wanashirikiana na Vyama vya jamii vya Misitu (CFA) kutekeleza miradi inayonufaisha jamii na mazingira katika sehemu kadhaa za nchi.

Aliongeza kuwa miradi hiyo imeundwa kupatia jamii ajira katika kutayarisha eneo, upanzi wa miche, kwekwe na kulinda eneo la mradi kwa muda ambao unadumu.

"Jamii pia inatoa miche ambayo inaiongezea mapato, na hivyo basi mipango hii ina manufaa kwa jamii, wizara na mazingira," alisema.

Waziri aliomba wakazi wanaoishi karibu na msitu wa Maasai Mau kulinda miche hiyo kutoka kuharibiwa na mifugo na watu ili ikue na kuongeza msitu.

Na *Ann Salaton (KNA)*

REPUBLIC OF KENYA

GAA GOVERNMENT ADVERTISING AGENCY

KENYA YEARBOOK EDITORIAL BOARD

**DESIGN AND EDITING OF MYGOV WEEKLY BY THE KENYA YEARBOOK EDITORIAL BOARD**
NHIF Building , 4th Floor, P.O. Box 34035-00100
Tel: 0202715390 / 0757029456
Email: info@kenyayearbook.go.ke
www.kenyayearbook.co.ke